MAKALA

**Uwekezaji Bandari na mkakati wa ajira milioni nane za Samia** Uk.12-13



**Programu ya Imarisha Uchumi na Mama Samia yazinduliwa Pwani** Uk. 6



Benki ya Dunia kuisaidia Tanzania utekelezaji wa miradi 14 ya kimkakati Uk.5


Mitandao @JAMVILAHABARI | Jamvi la habari | jamvihabari | +255676807684 | Email: jamvinews@gmail.com

GAZETI LAKO

# JAMVI LA HABARI

ISSN Na 2683 - 6548: Toleo Na. 2346 JUMATATU APRILI 22, 2024 Bei Tsh. 1000 Kenya Ksh. 60 www.jamvilahabari.co.tz


## RIPOTI MAALUM MIKOPO CHECHEFU

# MCHEZO MCHAFU

- **Wafanyabiashara** wakubwa wadaiwa kudhulumu mabenki kutumia mahakama
- **Wachota** mabilioni ya akiba za wateja na kujinufaisha, wagoma kulipa wakimbilia mahakamani mahakama yabariki
- **Mmoja** akwapua bilioni 40 TADB, akakwapua bilioni 70 Azania, akakwapua bilioni 110 Equity kisha akapiga bilioni 220 ujerumani
- **Mwengine** kachukua bilioni 15 NMB, akachukua bilioni 80 EQUITY akagoma kulipa akakimbilia mahakamani Jaji akampa ushindi anaendelea kutanua mitaani
- **Jaji** huyo huyo na kwa staili hiyo hiyo akampa ushindi mfanyabiashara mwingine aliyekwapua dola milioni 15 NMB
- **Jitihada** za Rais Dkt. Samia kuvutia uwekezaji zinazidi kukwamishwa, BOT, TIC, watakiwa kujipanga upya Uk.4



TADB Tanzania Agricultural Development Bank "The Farmers' Bank"

CRDB BANK Tunakusikiliza | NMB | EQUITY

**Wakulima wa tumbaku kulipwa ndani ya masaa 48** Uk.21

## Dkt Biteko amwakilisha Rais Samia mazishi ya Mkuu wa Majeshi Kenya

>> **Awataka** wakenya kuwa na subira katika kipindi hiki kigumu

>> **Mkuu** wa Majeshi ya Ulinzi (CDF) Jenerali Jacob Mkunda ashiriki maziko hayo Uk.3



# MCHEZO MCHAFU



NA. MWANDISHI WETU

JITIHADA za Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kukaribisha na kuhamasisha uwekezaji wa ndani na kutoka nje ya nchi kuja kuwekeza nchini unaelezwa kutiwa kigingi na tabia chafu inayozidi kuota mizizi ya baadhi ya wafanyabiashara wakubwa kushirikiana na baadhi ya majaji wa mahakama kuu wasio waaminifu kuyatapeli mabenki ya ndani na nje ya nchi kwa na hivyo kuwanyima fursa wafanyabiashara wadogo na wakati kushindwa kuaminiwa na kupata mikopo.

Orodha ya wafanyabiashara wanaotumia mahakama kutapeli na kudhulumu mabenki iliyofanyiwa uchunguzi na kuthibitishwa na gazeti hili, inaonyesha kuwa wengi kati ya wafanyabiashara hao wanajihusisha na biashara za Mafuta na ushafirishaji ambapo wastani wa shilingi za kitanzania Trilioni 1.3 wamekopa katika benki mbalimbali za ndani nan je ya nchi na kukataa kulipa kisha kukimbilia mahakamani ambako pia wanadaiwa kupata ushindi kwa njia zisizo za kawaida

Uchunguzi wa gazeti hili umebaini kuwa wafanyabiashara hao wanaoheshimika nchini wakionekana machoni mwa watu kuwa ni matajiri na wengine wakijionyesha kama wacha Mungu na wenye kumuogopa Mungu huku wengine wakijinasibu kama wana michezo na wawekezaji wakubwa wanaitumia mahakama hasa mahakama ya biashara kama kichaka chao cha kufanyia uhalifu huo wa kimkakati

''hebu fikiria, mtu amekwenda TADP amekopa bilioni 40, akaenda Azania benki akakopa bilioni 70, hajaishia hapo akaenda Equity benki akakopa bilioni 110, halafu akapanda ndege hadi ujerumani akavidanganya baadhi ya viwanda vya huko kuwa anaenda kuwekeza mafuta Kahama, nako wakamkopesha mali na mtaji wa zaidi ya bilioni 220, halafu anakataa kulipa mkopo makusudi kwa kukimbilia Mahakamani na Jaji anampa ushindi bila kuzingatia Ushahidi na ukweli kuwa hizo bilioni 220 za ndani na bilioni 220 alizochukua ujerumani zote kwa pamoja zinaingia kwenye deni la Taifa na kukataa kwake kulipa mkopo kunatunyima fursa sisi wafanyabiashara wadogo kuaminiwa''. Anasema Christopher Kabison mfanyabiashara wa vifaa vya simu Kariakoo

Kabison anaongeza kuwa kama Serikali haitachukua hatua za haraka kuingilia kati hali hii basi jitihada za Rais kutaka mabenki yakopeshe wafanyabiashara kwa riba nafuu zitabaki kuwa ndoto kwani hakuna benki itakayokuwa tayari kuendelea kupoteza mitaji yake huku mahakama zinazotarajiwa kuwa ni sehemu ya haki zikitumika kuhalalisha uchafu huo ''juzi nilikuwa napitia hukumu za mahakama, nimeshuhudia jaji mmoja amempa ushindi Stati oili ambaye alikopa dola milioini 26 equiti benki halafu akakataa kulipa, ukizipitia hizi hukumu unaweza ukajiuliza kama jaji wakati anatoa hukumu alikuwa sawa sawa ama ameonja kidogo..na jaji huyo huyo akahukumu hukumu kama hiyo kwa kampuni ya derina ambayo ilikopa zaidi ya bilioni 40 na kukataa kulipa. Sasa hapa tukisema mahakama inatumika kuhalalisha ujambazi dhidi ya watanzania tutakuwa tumeionea''. Aliongeza Kobisoni

Kwa mujibu wa taarifa na nyaraka ambazo gazeti hili linazo zinaonyesha kuwa miongoni mwa makampuni yanayoongoza kufilisi mabenki huku wakitumia mahaka ni pamoja na KOM GROUP ambayo imeweka kibindoni zaidi ya bilioni 440 na kukataa kulipa na kuziacha solemba benki za TADB,AZANIA pamoja na EQUITY sambamba na ujerumani

Wengine wanaoongoza genge la kukwamisha jitihada za Rais Dkt. Samia katika kukuza mitaji ya wafanyabiashara wadogo na wa kati kwa kukataa kulipa mikopo na kisha kukimbilia mahakamani na mahakama kuwapa hukumu za ushindi ni pamoja na kampuni ya TSN iliyozidhulumu benki za NMB na Equity, Derina Group iliyozidhulumu benki za CRDB na KCB huku BIG BON ikitajwa kuidhulumu benki ya NBC kama ambavyo Masasi construction inavyopambana kuidhulumu benki ya Equity kwa kutumia mahakama

Sambamba na kampuni hizo, nyingine ni Global Agency, State Oil inayomilikwa na Nilesh Suchak kama ilivyo kwa NAS HAULIERS na Continental reliable zinazotamba kuwadhulumu CRDB, NMB, NBC,EQUITY, KCB na nyinginezo

Ikiwa kitendo hiki cha wafanyabiashara hawa wakubwa kukopa na kuacha kulipa madeni kisha kukimbilia mahakamani na mahakama kuwapa ushindi kitaachwa kuendelee kuota mizizi kitapelekea Taifa kuwa na kikundi 'GANG' cha wafanyabiashara wanaoutawala Uchumi wa nchi na hivyo kuhatarisha amani ya Taifa

Kuwepo nje ya mzunguko wa benki hizi mabilioni hayo ya shilingi ni kiashiria kibaya katika ukuzaji wa Uchumi huku Gavana wa benki kuu akiombwa kuchukua hatua za haraka kuingilia sintofahamu hii inayozidi kushika kasi

''kama BOT hawatakuwa serious na kuingilia kati kunusuru hili jambo, benki zitafungwa hizi, ama zisipofungwa basi Uchumi utahama kutoka kuwa rasmi na kuwa Uchumi wa kihuni unaondeshwa na wahuni, lazima benki kuu iingilie kati haraka''. Alisema Juma Hamad mchambuzi wa masuala ya kiuchumi

Aliongeza kuwa katika Taifa lolote ambalo linaheshimu utawala wa sheria, ni nadra kwa wafanyabiashara kukopa halafu kukataa kulipa makusudi kisa tu kuna mahakama, hali hii inaweza kushawishi na wafanyabiashara wadogo nao kukataa kulipa na ikiwa wakashindwa mahakamani basi itasababisha hali ya sintofahamu

Gazeti hili linaendelea na jitihada za kuwatafuta wote waliotajwa kukapua mabilioni hayo na kukataa kulipa huku simu zao za mkononi zikiita bila kupokelewa.

Gazeti hili litaendelea kuweka wazi mchezo wote.

# Dkt Biteko amwakilisha Rais Samia mazishi ya Mkuu wa Majeshi Kenya

NA MWANDISHI WETU

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto Biteko, amemwakilisha Rais, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwenye mazishi ya aliyekuwa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama nchini Kenya Jenerali Francis Omondi Ogolla, aliyefariki kwa ajali ya helikopta tarehe 18 Aprili, 2024 eneo la Kaben Marakwet Mashariki mwa Kenya.

Akitoa salamu za Mhe. Rais amesema kuwa, Dkt. Samia anatoa pole kwa Rais wa Kenya, Dkt. William Ruto, Wakenya na Familia ya marehemu Jenerali Ogolla na kuwaombea kwenye kipindi hiki kigumu. "Mhe Rais amenituma niwape pole kwa msiba huu mkubwa hususani Majeshi ya Ulinzi na Usalama kwa kumpoteza kiongozi makini, shupavu, wa ngazi ya juu na kuwaomba muwe na moyo wa subira katika kipindi hiki kigumu" Amesema Mhe. Biteko

Aidha, amewaasa Wakenya kuyaishi yale ambayo Jenerali Ogolla ameyaishi katika kipindi chote cha uhai wake, akiwa anawatumikia wananchi wa Kenya, na kuongeza kuwa yawe somo kwa wote hususani kwa vijana.

Rais wa Kenya, Mhe. Dkt. William Ruto amewataka Wakenya kuwa na subira katika kipindi hiki ambapo Serikali imepoteza shujaa ambaye anatambuliwa kwa utendaji wake kama Mkuu wa Majeshi aliyeonyesha uwezo mkubwa katika utendaji kazi.

"Niwape pole Wakenya wote kwa msiba huu na niwaambie ningekuwa na uwezo wa kuchagua tena, ningemchagua Jenerali Ogolla kwani chini ya utendaji wake wa kazi, Jeshi la Kenya lilikuwa salama "Amesema Mhe. Dkt. Ruto.

Marehemu Jenerali Francis Omondi Ogolla alizaliwa Februari 12, 1962 katika Kaunti ya Siaya na alijiunga na jeshi la Kenya mwezi Mei 1984 na baadaye kutunukiwa cheo cha Luteni mwezi Mei 1985 ambapo alipangiwa kikosi cha Anga cha Moi na baadaye kupatiwa mafunzo ya Urubani.

Katika kipindi chote akiwa kwenye Jeshi la Kenya, Jenerali Ogolla alihudumu katika nyadhifa mbalimbali kwenye vikosi vya Anga hadi alipopandishwa cheo kuwa Jenerali na kuteuliwa kuwa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama wa Kenya (CDF) tarehe 28 Aprili, 2023.

Maziko hayo pia yalihudhuriwa na Makamu wa Rais wa Kenya Mhe. Rigathe Gachagua, Waziri Mkuu wa Kenya Musalia Mudavadi, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi (CDF) kutoka Tanzania Jenerali Jacob John Mkunda, Spika wa Bunge la Kenya Moses Watengala Masika, wakuu wa vikosi vya majeshi ya Ulinzi na Usalama nchini Kenya, Malawi, Uganda Rwanda, Namibia, Burundi.



# Simbachawene asisitiza wanafunzi kushiriki katika mapambano ya rushwa, dawa za kulevya

NA MWANDISHI WETU

SERIKALI imesema itaendelea kushirikiana na ngazi zote za elimu katika kupambana na Rushwa na Dawa za kulevya.

Hayo yalibanishwa jijini Dodoma na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe.George Simbachawene, wakati akizidua mashindano ya mdahalo kwa shule za msingi Sekondari,Vyuo vya kati na Vyuo Vikuu kuhusu Madhara ya Rushwa,Matumizi ya Dawa za Kulevya,Haki za Binadamu na Utawala Bora.

Alisema serikali za awamu zote zimefaikiwa kwa kiasi kikubwa kupambana na maadui watatu ambao ni ujinga, umaskini maradhi kwa Watanzania.

"Sasa wameibuka maadui wengine watatu ambao ni rushwa, dawa za kulevya na maadili ambao kuna kazi kubwa ya kufaya kuhakikisha tunatokomeza, hili sio suala la kuachia serikali pekee ni vyema kila mwananchi akashiriki kikamilifu,"alisema

Aliogeza kuwa:"Leo ninafurahi kuzindua mdahalo huu kwa shule na vyuo vya Dodoma kuhusu masuala ya rushwa ni jambo jema kwasababu ndio msingi imara wa kuandaa viongozi wazalendo na ningetamani kuona kitu kama hiki kiafanyika nchi nzima,".

Simbachawene alimpongeza Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Jabir Shekimweli kwa kuandaa midahalo hiyo ambayo imekuwa na manufaa makubwa kwa wanafunzi wa ngazi zote za elimu.

Kwa upande wake Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Dodoma Bw.John Joseph alisema wanaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu athali za rushwa hasa katika miradi ya maendeleo ambayo inatekelezwa katika maeneo yao.

Alisema pia wameedelea kuanzisha klabu za wapinga rushwa kuanzia shule za msingi hadi vyuo lengo ni kuongeza mtandao wa kupokea taarifa za rushwa na kutoa elimu kwa kudi hilo la vijana ambao ndio nguvu kazi ya Taifa.

"Tunaendelea kufungua klabu za wapinga rushwa lengo ni kuhakikisha tunalifikia kundi kubwa la vijana ambao ndio nguvu kazi ya Taifa ambapo tunaamini tukiwaelimisha wao tutakuwa tumeelimisha Taifa,"alisema

Naye Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Jabir Shekimweri alisema lengo la kuanzisha midahalo hiyo ni kuhakikisha watu wanapata uelewa wa kutosha kuhusu athali za rushwa.

"Watu wengi wamekuwa wakikosa haki zao za msingi kwasababu ya vitendo vya rushwa na ndio kitu kikubwa kilichonisukuma kuanzisha jambo hili ambalo hadi sasa limeonyesha matunda makubwa,"alisema

Awali Mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Bunge Mariamu Minja alisema midahalo hiyo imekuwa na manufaa kwao kwasababu inawafundisha ni kwa namna gani wanatakiwa kuwa wazalendo.

"Tunamshukuru Mkuu wa Wilaya ya Dodoma kwa kuja na wazo hilo kiukweli limekuwa na manufaa kwetu tunaomba isiishie mjini hata wanafunzi walioko vijijini nao wapate fursa ili wapate elimu na uelewa wa kutosha kuhusu masuala ya rushwa,"alisema

# Dkt. Gwajima afungua mkutano wa 21 wa MEWATA, asisitiza umuhimu kujenga msingi ya afya ya watoto

NA MWANDISHI WETU

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Vikundi Maalum Mhe. Dkt. Dorothy Gwajima amekitaka Chama cha Madaktari Wanawake Tanzania (MEWATA) kuongeza nguvu katika jitihada za kukabiliana na mila na desturi kandamizi katika jamii kwa ajili ya kuleta maendeleo stahimilivu kwa wanawake, wanaume pamoja na watoto.

Akizungumza jana Aprili 21, 2024 jijini Dar es Salaam wakati akifungua mkutano mkuu wa mwaka wa MEWATA uliofanyika katika hoteli ya New Afrika, Mhe. Dkt. Gwajima amesema kuwa wakati umefika kwa MEWATA kufanya kazi na wizara hiyo katika kuhakikisha wanatengeneza misingi imara ya watoto wa kike kwa kupata afya bora ili waweze kufanya vizuri na kuleta ushindani.

Dkt. Gwajima amesema kuwa ni vizuri kuweka mikakati ya kuendelea kuunga mkono juhudi zinazolenga kuwawezesha wanawake kupata huduma za afya na kukomesha vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

"Ni muhimu kufanya kazi kwa ushirikiano katika utoaji wa huduma kwa wahanga wa ukatili wa kijinsia kwa kuwezesha ujenzi wa vituo vya wanawake pamoja na vituo vya ushauri nasaha kwa walionusurika" amesema Dkt. Gwajima.

Amebainisha kuwa mujibu wa Ofisi ya takwimu ya Utafiti wa Demografia na Afya 2015 – 2016 zinaonesha asilimia ya 40 ya wanawake wenye umri kati 15 – 49 wamefanyiwa ukatili wa kimwili, huku asilimia 17 wamefanyiwa ukatili wa kijinsia.

"Jamii zetu bado zinakabiliwa na changamoto ya mila na desturi kandamizi ambazo zinazowazuia wanawake na watoto kufikia ndoto zao na kutoa mchango wao katika ustawi wa jamii na Taifa kwa ujumla" amesema Dkt. Gwajima.

Rais wa Chama cha Madaktari Wanawake Tanzania (MEWATA) Dkt. Zaituni Bokhary, amesema kuwa kuna changamoto nyingi zinawapata wanawake lazini wanashindwa kusema kutokana na mila potofu zilizopo kwa baadhi ya jamii.

Dkt. Bokhary amesema kuwa ili kufika malengo tarajiwa wamejipanga kutoa elimu kuhusu afya ya mwanamke katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo vijijini.

"Tupo tayari kufanya kazi kwa ushirikiano kwa kuweka mipango rafiki katika kuhakikisha tunawafikia walengwa na kuwapatia elimu hasa maeneo ya vijijini ambapo kunaonekana kuna uhitaji mkubwa" amesema Dkt. Bokhary.

Nae Makamu wa Rais wa Chama cha Madaktari Wanawake Tanzania (MEWATA) Dkt. Marry Sando, amesema kuwa kupita taaluma zao kwa kushirikiana na wizara wataweza kutoa msaada na kutengeneza jamii iliyokuwa na mstali mwema.

Amesema kuwa katika mkutano watapata fursa ya kujadili kwa namna gani wanaweza kutoa mchango wa kitaaluma katika afya ya mama na mtoto na jamii kwa ujumla.

# Afisa Mtendaji Mkuu Benki ya NMB ataka vijana wafundishwe masuala ya fedha na bajeti mapema

NA MWANDISHI WETU, BUKOBA

AFISA Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB Ruth Zaipuna ametoa ushauri kwa wazazi na walezi nchini kuwafundisha mapema watoto wao masuala ya fedha na upangaji wa bajeti ili kuwawezesha kuishi kutokana na uhalisia wa vipato vyao.

Zaipuna ailtoa ushauri huo katika hotuba yake wakati wa mahafali ya kidato cha sita katika shule za sekondari za Kaizirege na Kemebos zilizopo mjini Bukoba mwishoni mwa wiki.

Alisema watoto wakipata elimu ya masuala ya fedha mapema watakuwa waadilifu,wataweza kupanga maisha yao kwa kuzingatia bajeti inayotokana na vipato vyao hata baadaye kuwekeza kwa uadilifu kwenye miradi ya kiuchumi.

"Tuanze kuwajengea vijana wetu uelewa wa masuala ya fedha wakati huu ambao bado ni mapema,wakipata elimu ya masuala ya fedha watakaweza kupangalia vyema maisha "alisema Zaipuna

Pia alisema ili kulisaidia kundi hilo,benki ya NMB ilianzisha jukwaa maalum la vijana liitwalo"Go na NMB"ambapo wanafundishwa masuala ya fedha na jinsi ya kujiwekea akiba na kutumia huduma mbalimbali za kidijitali zinazotolewa na benki hiyo.

Zaipuna katika hafla hiyo alitoa wito kwa vijana kujiunga na jukwaa hilo kwa ajili ya kupata maarifa ya masuala ya kifedha ambayo yatawasaidia katika safari ya maisha yao huku akiwakumbusha kuwa kutokana na mabadiliko mbalimbali hasa ya kitekinolojia,wanatakiwa kujifunza mambo mengi,kuwa wadadisi na wabunifu.

Aidha alisema benki ya NMB imeendelea kuunga mkono ukuaji wa sekta ya elimu hapa nchini,ikiwa ni pamoja na kutoa ufadhili wa masomo na vifaa kwa wanafunzi wanaojiunga vyuo vikuu wanaotoka kwenye familia zenye uwezo mdogo ambao wamefaulu vizuri.

Alisema zaidi ya wanafunzi 130 wanaebdelea kunufaika na ufadhili huo.

Katika risala yao kwa niaba ya wahitimu wa shule zote mbili za Kaizirege na Kemebos,wanafunzi Zubeda Kinono na Avin Mutegeki walisema matumaini yao ni kufanya vizuri katika mitihani yao na kujiunga vyuo vikuu.

Walisema kama walivyovumilia changamoto katika safari yao,pia watahakikisha wanaonyesha juhudi katika masomo yao kwenye Taasisi za Elimu ya Juu ili baadaye waweze kulitumikia Taifa kwa uadilifu kupitia sekta mbalimbali.

# Meya Kumbilamoto asifia wahudumu sekta ya afya

NA MWANDISHI WETU

TAKRIBAN wahudumu wa Afya ngazi ya Jamii 200 katika Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam wametakiwa kuendelea kuonyesha juhudi katika kuwahudumia wananchi katika Maeneo yao Ili kuweza kuwaondolea changamoto mbalimbali.

Kauli hiyo imetolewa jana jijini Dar es salaam na Meya wa Jiji la Dar es salaam Omary Kumbilamoto katika hafla ya kukabidhi vitendea kazi kwa wahudumu wa Afya ngazi ya jamii ambapo imekwenda na Kauli Mbiu isemayo wahudumu wa Afya ngazi ya jamii Nyumba kwa Nyumba hatuachi Mtu Mpaka kieleweke.

Kumbilamoto licha ya kuwapongeza wahudumu hao wa Afya kutokana na kuanza kazi kwa kujitolea amesema kuwa ni vyema wakaendelea kuwasaidia wananchi wa ngazi ya Chini.

"Hawa wahudumu wetu wanavifua kwa sababu hawatoi siri za wagonjwa wanaowasaidia jambo ambalo linaendelea kuongeza uaminifu naona yao"amesema Kumbilamoto

Awali Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam Zaitun Hamza amesema kuwa wahudumu wa Afya wanatembea kifua mbele kutokana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Samia Suluhu Hassan kwa kuipa kipaumbele sekta ya Afya.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu uchumi na Huduma za Kijamii katika Jiji la Dar es salaam Saad Khimji amesema wataendelea kujadili namna ya wahudumu hao kunufaika na shughuli zao kwani wanajitoa na kunusuru mambo mengi kwenye jamii.

Nao baadhi ya wahudumu wa Afya ngazi ya jamii akiwemo Abdallah Ngobedi pamoja na Masha Abdallah Jumbe wameipongeza serikali kwa kuonyesha umuhimu kwenye sekta hiyo kwa kuwapatia vifaa hivyo ambavyo vitakwenda kuwasaidia katika shughuli zao.



*Afisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna (katikati) akimkabidhi Cheti cha kuhitimu kidato cha sita kwa mmoja wa wanafunzi wa wa Shule za sekondari Kaizirege na Kemobos katika mahafali ya shule hizo mkoani Bukoba ambapo alikuwa Mgeni Rasmi wa shuguli hiyo. Kulia ni Mkurugenzi wa shule hizo, Eusto Kaizirege.*

# Zanzibar washiriki wiki ya maabara kidunia

NA MWANDISHI WETU

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi amewataka wataalamu wa Maabara kuvifanyia utafiti vitu wanavyovichunguza ikiwemo maradhi ili kuyadhibiti kwa njia za kisayansi.

Akisoma hotuba ya Rais Mwinyi katika kilele cha wiki ya Maabara Duniani huko Hoteli ya Golden Tulip Uwanja wa Ndege Zanzibar alipomwakilisha, Waziri wa Afya Zanzibar Nassor Ahmed Mazrui amesema kufanya hivyo kutasaidia taasisi kudhibiti maradhi na kuzielekeza njia zinazoshauriwa kirahisi kutokana na kuwepo na ushahidi wa Kisayansi.

Aidha amewataka wataalamu hao kuongeza nguvu kwenye Taasisi za Tafiti ikiwemo za Taaisi ya Afya ya Binaadamu (ZAHRI), Utafiti wa Mifugo (ZALIRI), Taasisi ya Utafiti wa Safayansi ya Baharini (ZAFIRI) ili kuweza kufikia malengo yaliokusudiwa.

Amefahamisha kuwa Maabara zote zina mchango mkubwa kwa maendeleo mbalimbali ikiwemo ya afya na huduma zinazotolewa kwa wananchi, hivyo Serikali itaendelea kuimarisha Maabara zote ili kuweza kuendeleza kazi za uchunguzi wa maradhi, vinasaba, kemikali, pamoja na vyakula.

Akizungumzia Sera ya Maabara Zanzibar, amesema ni jambo zuri kwani utekelezaji wa kazi za vipimo hasa zinapokuwa zinatekelezwa na wadau tofauti ni vyema kuwepo na Miongozo itakayosaidia kulinda mipaka ya kiutendaji, ubora na viwango vinavyojali maslahi mapana ya wanaotegemea huduma kwenye Taasisi hizo.

Aidha amewasisitiza kushirikiana na kufanya kazi na Viongozi pamoja na mashirika ya kimataifa yanayoshughulikia maendeleo kwa lengo la kuleta maendeleo ya kweli kwa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla. Hata hivyo, amewatakaWataalamu hao kufanya mapitio ya mipango kazi yao kila robo ya mwaka ,miezi sinta na mwaka ili kuweza kujifanyia tathmini ya mafanikio na kuzitafutia ufumbuzi wa haraka changamoto zinazowakabili katika utekelezaji wa majukumu yao.

"Tusisubiri mpaka wiki ya maadhimisho ya maabara ndio mukaanza kufanya kazi hivyo hatuawaza kufikia malengo wa kupata maendeleo ya kweli kama tunavyojua Serikali inatuamini na inatutegemea kupata mambo mazur kutoka kwetu." alisema Kiongozi huyo.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu Wizara ya Afya Dkt. Amour Suleiman amesema lengo la maadhimisho ya wataalamu wa maabara Zanzibar ni kuungana na wataalamu wengine Duniani na kuona umuhimu wa kazi za Ki –Maabara katika kutoa huduma kwa jamii.

# Benki ya Dunia kuisaidia Tanzania utekelezaji wa miradi 14 ya kimkakati

NA BENNY MWAIPAJA, WASHINGTON D.C

WAZIRI wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, ameishukuru Benki ya Dunia kwa kuidhinishia Tanzania miradi 14 ya maendeleo yenye thamani ya zaidi ya dola za Marekani bilioni 3.87, kupitia mpango wa Benki hiyo wa utoaji mikopo na misaada (IDA-20), zilizoelekezwa katika miradi ya sekta za elimu, afya, hifadhi ya mazingira, miundombinu, nishati na Tanzania ya Kidigiti.

Dkt. Nchemba ametoa shukrani hizo wakati akizungumza na Makamu wa Rais wa Benki ya Dunia, anayesimamia nchi za Kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika, Bi. Victoria Kwakwa, wakati wa Mikutano ya Kipupwe (Spring Meetings) ya Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), jijini Washington DC, Marekani.

Alisema kuwa miradi hiyo 14 ni kati ya miradi 25 ya kimkakati yenye thamani ya dola za Marekani bilioni 5, ambayo Serikali iliiwasilisha kwenye Benki hiyo kwa ajili ya kupatiwa fedha ili iweze kutekelezwa na kuchangia kuchochea ukuaji wa uchumi jumuishi, maendeleo ya nchi na kupunguza umasikini kupitia malengo yaliyowekwa katika Dira ya Taifa ya 2025.



*Ujumbe wa Tanzania (kushoto) ukiongozwa na Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), ukiwa katika kikao na Ujumbe wa Benki ya Dunia ulioongozwa na Makamu wa Rais wa Benki ya Dunia, anayesimamia nchi za Kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika, Bi. Victoria Kwakwa, wakiwa katika kikao chao kilichofanyika katika Ofisi za Makao Makuu ya Benki hiyo, jijini Washington D.C, nchini Marekani, wakati wa mikutano ya Majira ya Kipupwe (Spring Meetings) ya Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) yenye kauli mbiu ya "Vision to Impact" inayoendelea jijini humo.*

Dkt. Nchemba aliishukuru pia Benki hiyo kwa kutoa Awamu ya Kwanza ya kiasi cha dola za Marekani milioni 500 kati ya kiasi cha dola milioni 750, mwezi Desemba mwaka 2023, kwa ajili ya kuchangia Bajeti ya Serikali, ili kukabiliana na athari za Uviko-19 na vita vinavyoendelea baina ya Ukraine na Urusi kwa kuwekeza kwenye miradi inayochochea uchumi na huduma za jamii.

Aidha, Dkt. Nchemba alishukuru Benki ya Dunia kwa kuahidi kusaidia ujenzi wa mradi wa Kikanda wa Reli ya Kisasa (SGR) utakaoziunganisha nchi za Tanzania, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, mradi ambao ni muhimu kwa ajili ya kuchochea biashara, ukuaji wa uchumi, kuboresha mtandao wa miundombinu ya usafiri na usarishaji, kudhibiti mabadiliko ya tabianchi na kukuza ajira katika ukanda huo.

Akizungumza katika Mkutano huo, Makamu wa Rais wa Benki ya Dunia anayezisimamia nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika, Bi. Victoria Kwakwa, aliipongeza Tanzania kwa hatua mbalimbali inazozichukua katika kusimamia uchumi na maendeleo ya wananchi wake na kwamba mafanikio hayo yanapaswa kuigwa na nchi nyingine.

Aliahidi kuwa Benki ya Dunia iko tayari kuendelea kuisadia Tanzania ili iweze kufikia malengo yake ya maendeleo kwa kuipatia fedha na utaalam kwa kuziwezesha sekta muhimu za uzalishaji na huduma za jamii kushamiri kikiwemo kilimo, nishati, uchumi wa kidigiti, hifadhi ya mazingira, maji, elimu na ujenzi wa wa miundombinu ya usafirishaji.

Bi. Kwakwa aliahidi pia kuwa Benki ya Dunia itashiriki kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Reli ya Kisasa ya SGR ya Kikanda itakayotekelezwa katika nchi tatu za Tanzania, Burundi na DRC kwa kuwa mradi huo ni muhimu katika kukuza biashara na uwekezaji katika Ukanda mzima wa nchi za Afrika.

Bi. Kwakwa alisema pia kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi 15 zilizochaguliwa na Benki ya Dunia kwa ajili ya kunufaika na mpango wa biashara ya kuuza hewa ya ukaa duniani ambapo Benki hiyo itatoa fedha za kuimarisha sekta ya misitu ili fedha zitakazopatikana kupitia biashara hiyo ya hewa ya ukaa ziweze kusaidia maendeleo ya nchi.


# TANGAZA NASI SASA

*Unatamani kukuza biashara yako kutoka hapo ilipo kuwa kubwa na yenye mantiki zaidi?*

- *Unatamani kuongeza kipato, uelewa na upana wa shughuli zako za kila siku?*
- *Je unataka kuwafikia wateja wako ndani na nje ya nchi kwa kiasi kikubwa ili kukuza biashara na huduma yako?*
- *Fahamu kwamba JAMVI LA HABARI na mitandao yake ya kijamii kama Youtube, Instagram, Facebook, Website na Twitter hutembelewa na maelfu ya wasomaji kila siku Duniani kote.*
- *Hivi unafahamu kuwa JAMVILAHABARI kwa sasa ni moja kati ya Media chache zinazo ongoza kwa kutoa taarifa sahihi na kwa wakati zinazotokea nchini na Duniani kwa ujumla?*

*TANGAZA SASA NA JAMVI LA HABARI KWA PUNGUZO KUBWA LA BEI UPATE MATOKEO YA HARAKA.*

*Kwa matangazo yote kama vile minada, kupotelewa kwa vyeti vya shule, matangazo ya makampuni, nafasi za kazi, zabuni za kazi, maonyesho, dawa za asili, taasisi za elimu, taasisi za dini na mengine mbalimbali mbali mbali.*

*Ni rahisi sana, wasiliana nasi kupitia Whatsap namba +255659555744 au tupigie katika +255743777778 au +255659555744 GHARAMA ZETU NISAWA NA BUREE JAMVILAHABARI; TUMECHAGUA KUKUHUDUMIA www.jamvilahabari.co.tz*

# Mabalozi wa Tanzania wajifungia Kibaha, kutafakari na kujipanga upya

NA HAFIDH KIDO

MABALOZI wanaowakilisha Tanzania katika nchi mbalimbali duniani na Wakuu wao wa utawala wamejifungia katika Chuo cha Uongozi Cha Mwalimu Julius Nyerere mjini Kibaha kwa siku 4 kuanzia tarehe 20 hadi 24 Aprili 2024.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mhe. January Makamba (Mb) ametaja sababu za kujifungia huko kuwa ni pamoja na kukutana kama familia ya wanadiplomasia wa zamani na wa sasa ili kubadilishana uzoefu wa namna bora ya kutekeleza Sera ya Mambo ya Nje ambayo imejikita katika diplomasia ya uchumi.

Mhe. Makamba alisema kazi ya diplomasia ni moja ya kazi muhimu duniani na kupitia kazi hiyo Tanzania imejitangaza na kusikika, hasa kupitia misimamo yake na umahiri wa wanadiplomasia iliyokuwa nao.

Hivyo, vikao hivyo ni muhimu kwa ajili ya kupata mwendelezo huo, kwani vinatoa fursa ya kutafakari upya na kupanga mikakati ya namna bora zaidi ya kutekeleza majukumu ya Wizara hiyo ambayo ni moja ya nguzo muhimu ya ukuaji wa uchumi nchini.

Alisema mfumo wa kikao hicho ambao ni tofauti kabisa na mifumo ya vikao vilivyofanyika miaka ya nyuma ni kwamba wanadiplomasia watapewa fursa ya kubadilishana kinaga ubaga changamoto wanazokabiliana nazo katika utekelezaji wa majukumu yao, kutafakari kwa pamoja namna bora ya kuzitafutia ufumbuzi na baadaye kuweka mpango kazi wa utekelezaji.

Aliwahakikishia kuwa Serikali itajitahidi kutoa nyenzo ilizo nazo ili kazi hiyo muhimu iweze kutekelezwa na kuleta matokeo chanya yanayotarajiwa.

"Tutafakari majukumu yetu, masuala mahususi ya kuzingatia pamoja na kutathimini nyenzo zetu za utekelezaji ili wote tuwe katika uelewa na mweleko mmoja wa kufanikisha malengo ya Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mama yetu, Mwana diplomasia namba moja, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan". Mhe. Makamba alisema.

Warsha hiyo ya Mabalozi inajumuisha pia Makatibu na Naibu Makatibu Wakuu wa Wizara wakiongozwa na Balozi Dkt. Samwel Shelukindo, Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na baadhi ya wadau wanaoshirikiana kwa karibu na Wizara katika utekelezaji wa majukumu ya Diplomasia.

# Programu ya Imarisha Uchumi na Mama Samia yazinduliwa Pwani

NA MWANDISHI WETU, PWANI

BARAZA La Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) limezindua programu kabambe ya 'Imarisha Uchumi na Mama Samia' lenye lengo la kuwawezesha wanawake, vijana na makundi maalum kujiunga na majukwaa ya kiuchumi ili kujishughulisha na ujasiriamali ili kujikwamua katika umasikini.

Akizungumza kwenye uzinduzi rasmi wa programu hiyo ya 'Imarisha Uchumi na Mama Samia' mjini kibaha juzi , Mshauri wa Rais wa Mambo ya Wanawake na Makundi maalum, Bi Sophia Mjema alisema kwamba progaramu hiyo maalum inafungua milango kwa wanawake, vijana na makundi maalum kujisajili na kuingia kwenye mfumo wa kieletroniki.

Alisema programu hiyo itawawezesha makundi hayo yote tajwa kuweza kupatikana kwa taarifa zao rasmi serikalini za kibiashara ili kwenda sambamba na utekelezaji wa sera ya kitaifa ya uwezeshaji wananchi kiuchumi.

Bi Mjema aliongeza kwamba mfumo huo wa kidigitali ambapo utaweka kanzidata na kupata takwimu ya idadi ya majukwaa ya kiuchumi ya wanawake ambapo watapata fursa ya kubadilishana uzoefu, kupanua wigo wa biashara na fursa mbalimbali.

"Rais wetu mama Samia Suluhu Hassan akiwa makamu wa rais aliwezesha uanzishwaji wa Jukwaa la wanawake kiuchumi ili kuweza kumkwamua mwanamke kutoka kwenye umasikini na aweze kujishughulisha na shughuli za uzalishaji mali na kushiriki kwenye shughuli za uchumi na biashara kwenye nchini yao," alisema Bi Mjema

Alisema kwamba ni nafasi ya wanawake kuchangamkia fursa zitakazotakana na programu hiyo kwa kuwahi kujiandikisha kwenye mfumo huo maalum ili kuweza kujulikana rasmi na serikali kuweza kupata nafasi ya kuwezeshwa kiuchumi na kupata fursa ya kupata ruzuku na mikopo kutoka kwenye taasisi za kifedha na mifuko ya ruzuku.

Bi Mjema aliongeza kwamba kwa sasa dunia ipo kwenye sayansi na tekonolojia ndio maana baraza hilo limeamua kuja na programu hii ya kieletroniki ili kuweza kupata takwimu sahihi ya wanawake na vijana nchini nzima lakini pia kutoa mwamko wa matumizi ya teknolojia kwa wajasiriamali hapa nchini.

Alifafanua kwamba ni muhimu pia kwa baraza kuendelea kuhamasisha wanawake kuendelea kujisajili na kuwatajarisha watanzania kushiriki kwenye biashara za ushindani na kuwajengea uwezo na mafunzo kuhusu shughuli mbalimbali za kiuchumi hapa nchini.

"Ukienda China kuna maeneo maalum yametegwa kwa ajili ya huduma na bidhaa fulani , nina imani ipo siku tutafika huko kwa sasa kibaha ni sehemu maalum ya viwanda tutumie fursa hiyo ya viwanda kuweza kufanya biashara na kutoa huduma kwenye viwanda," aliongeza

Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) Bi Beng'i Issa alisema kwamba programu hiyo ni maalum kwa ajili kuwatambua na kuwajengea uwezo wa kiuchumi wanawake , vijana na makundi maalum ili kuendana na maono ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuwakwamua wanawake kiuchumi hapa nchini.

Alisema kwamba jukumu moja la baraza hilo ni kuwawezesha wananchi kwa kuwapa taarifa, ujuzi kwa maana ya kutoa mafunzo mbalimbali na kuwaunganisha na taasisi za kifedha na mifuko ya ruzuku kwa ajili ya kupata fedha ili kuweza kufanya biashara zao kwa ufanisi zaidi.

*Sehemu ya Mabalozi wakifurahia jambo wakati Waziri Makamba akizungumza kwenye kikao cha maandalizi kuelekea warsha ya Mabalozi iliyoanza tarehe 21 Aprili 2024 mjini Kibaha, Pwani*



# Mkaguzi mkuu wa ndani kuongeza usimamizi wa mapato na matumizi

NA PETER HAULE, WF. ARUSHA

MKAGUZI Mkuu wa Ndani (IAG), Bw. Benjamini Magai amesema ofisi yake itafanya mabadiliko makubwa katika taratibu za ukaguzi katika maeneo ya mapato na matumizi kutokana na mafunzo muhimu waliyoyapata katika Mkutano wa 10 wa Shirikisho la Taasisi za Wakaguzi wa Ndani Afrika (AFIIA)

Hayo aliyasema jijini Arusha wakati wa kuhitimisha siku tano za Mkutano wa 10 wa Shirikisho hilo uliowakutanisha zaidi ya wajumbe 1200 kutoka nchi 27 za Afrika na nje ya Afrika.

Bw. Magai alisema kuwa kutokana na kukua kwa teknolojia nchi yetu inatumia mifumo ya kielektroniki katika matumizi na ukusanyaji wa mapato, hivyo katika eneo hilo kumekuwa na vihatarishi vya udukuzi, kama nchi inatakiwa kujipanga vizuri kupitia wakaguzi wake.

"Tumejifunza mambo mengi katika mkutano huu, kuna baadhi ya maeneo inawezekana yalikuwa hayatekelezwi kwa ufanisi, kwa sasa tunakwenda kuongeza tija zaidi kwa kuwa wakaguzi wetu sasa wanaweza kufanya kaguzi za kitaalamu zaidi kuliko ilivyokuwa awali", alisema Bw. Kigai.

Bw. Magai amesema kuwa Mkutano huo wa 10 wa Wakaguzi wa Ndani Afrika uliofunguliwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, umechochea hamasa ya kufanyakazi kwa weledi mkubwa unaoambatana na matumizi ya teknolojia ili kuhakikisha taratibu muhimu katika eneo la ukusanyaji mapato, matumizi na pia mazingira na uatawala bora zinafuatwa.

Akizungumzia kuhusu ukaguzi wa mazingira, Bw. Kigai alisema kuwa ni eneo jipya ambalo wakaguzi waliona sio muhimu lakini kwa sasa limepewa uzito mkubwa ukizingatia kwa sasa kuna athari kubwa za mabadiliko ya tabianchi yanayosababisha mafuriko, joto na maporomoko ya ardhi jambo ambalo mkaguzi anatakiwa kuwa na jukumu muhimu katika kuhakikisha taasisi zote za umma zinajipanga katika kukabiliana na na masuala hayo.

Aidha alisema kuwa mkutano huo ulijumuisha eneo la Utawala bora na masuala ya kitaalamu katika eneo la ukaguzi ambao ulifanyika kwa siku mbili na kufuatiwa na Kongamano lilochukua siku tatu ambalo lilijikita katika masuala ya ukaguzi wa ndani.

# TAHARIRI

## Jukumu letu vijana kueleza na kufafanua mipango ya Rais Samia

KILA zama na kitabu chake, haya yalipata kuzungumzwa na wataalamu kadhaa katika nyanja mbalimbali za fasihi kwa lengo la kujenga uelewa wa mambo.

Vilevile aliyepata kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika awamu ya pili, Hayati Mzee Ali Hassan Mwinyi alipata kuyasema haya na kuongeza kuwa maisha tunayoishi ni kama hadithi basi tuwe hadithi njema kwa watakaosimuliwa.

Maana yake, kwa sasa Rais Samia Suluhu Hassan najaribu kujenga uelewa na kujiamini kwa Watanzania hasa vijana katika Nyanja mbalimbali za kimaendeleo.

Hata hivyo, huenda kuna watu hawajamuelewa au wamemuelewa lakini hawana uhakika na kile anachokiamini Rais Samia.

Hivyo, vijana ambao kwa sasa tunazo nguvu na maarifa tunahitajika kumsaidia Rais Samia katika kuyaelewa na kuyasambaza yale anayoyaamini kwa faida ya sasa na baadaye kwa taifa letu.

Tukumbuke kuwa sisi ndio tutakaokuwa watu wa kujibu maswali ya watoto na wajukuu wakati huo miaka mingi imeshapita na hakuna kilichofanyika katika namna yoyote ya kukuza uchumi wa Tanzania na kuondokana na matatizo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Jamvi la Habari, tukiwa mstari wa mbele katika kuyaeleza, kuyafafanua na kuyasambaza mawazo ya serikali yetu iliyopo madarakani kwa sasa, tunaamini kuwa kila mmoja katika sisi tunalo jukumu la kusimakia maono ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuifikia Tanzania mpya.


## BODI YA UHARIRI

Mhariri Mkuu - 0713 593 894
Idara Ya Matangazo/Masoko - 0743 777 778, - 0659 555 744
Idara Ya Usambazaji - 0676807684, - 0787 288 160

Gazeti hili hutolewa na **ZABA INVESTMENTS**
S. L. P 78862, Dar es Salaam
**Tel:** +255 676 807684, 255 743 777778
**Email:** jamvinews@gmail.com
www.jamvilahabari.co.tz




*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango akiwasili katika Uwanja wa Ndege wa Pemba, Zanzibar ambapo anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika Ufunguzi wa Skuli ya Sekondari Maziwang'ombe iliyopo Wilaya ya Micheweni Mkoa wa Kaskazini Pemba jana tarehe 21 Aprili 2024 ikiwa ni Shamrashamra za Maadhimisho ya Miaka 60 ya Muungano.*

UCHAMBUZI

## Bwawa la Julius Nyerere halihusiani na mafuriko ya Rufiji

PALITOKEA mafuriko katika Wilaya ya Rufiji mkoani Pwani ambapo wananchi zaidi ya 1,000 waliathirika kwa namna mbalimbali ikiwemo mazao yao kuharibiwa na wengine kupoteza makazi.

Baadhi ya vyombo vya habari vimeripoti kuwa mafuriko ya Rufiji ni matokeo ya kufunguliwa kwa maji katika Bwawa la Mwalimu Nyerere, jambo ambalo halina ukweli wowote.

**JE MAFURIKO YA RUFIJI YAMESABABISHWA NA NINI?**

Mvua za El-Nino zinazoendelea kunyesha zimesababisha mafuriko kwenye baadhi ya maeneo kama vile Rufiji, Kilombero, Mvomero, Kilosa, Mlimba, Liwale, Mbarali n.k.

Ukiondoa Wilaya ya Rufiji ambayo maji ya bwawa la Mwalimu Nyerere yanapita kuelekea Bahari ya Hindi, wilaya zingine zilizoathirika na mafuriko hazipitiwi na maji ya bwawa hilo. Kwa mfano Mvomero haipitiwi na maji kutoka bwawa la Mwalimu Nyerere lakini mafuriko yameathiri hadi kiwanda cha sukari Mtibwa ambacho kimesimamisha uzalishaji.

Wilaya ya Rufiji ina historia ya kukumbwa na mafuriko mara kwa mara kutokana na sehemu kubwa ya wilaya hiyo kuwa bondeni. Mwaka 1997, 2000, 2003, na 2011 wilaya hiyo ilikumbwa na mafuriko makubwa yaliyosababisha uharibifu wa mali na baadhi ya watu kupoteza maisha. Wakati huo bwawa la Mwalimu Nyerere halikuwepo. Kwa hiyo kusema kwamba bwawa hilo limesababisha mafuriko si kweli. Je miaka mingine mafuriko yalitokana na bwawa gani?

Wananchi kuvamia na kufanya shughuli za kibinadamu maeneo ya mkondo wa mto. Kwanza ieleweke kwamba kiwango cha juu cha maji katika mto Rufiji ambacho kimewahi kurekodiwa ni mita za ujazo 13,000 kwa sekunde. Kiwango hicho kilirekodiwa Mei 1974. Kiwango cha maji katika mto Rufiji kwa Machi na Aprili, 2024 ni mita za ujazo 8,444 kwa sekunde.

Maana yake ni kwamba kiwango cha maji katika mto Rufiji mwaka huu hakijafikia makadirio ya juu kama ilivyokua mwaka 1974. Sasa kwa nini mafuriko yametokea? Kwa nini kiwango cha mita za ujazo 13,000 mwaka 1974 hakikusababisha madhara makubwa kama kiwango cha mita za ujazo 8,444 mwaka huu?

Jibu ni kwamba wananchi wamevamia eneo la mkondo wa mto na kufanya shughuli za kibinadamu ikiwemo kulima na kujenga. Serikali ilipoanza kujaza maji kwenye bwawa la Mwalimu Nyerere mwaka 2022, maji yote ya mto Rufiji yalizuiwa.

Kwa hiyo hakukua na maji yaliyotiririrka kuelekea baharini. Matokeo yake wananchi walisogea kwenye mkondo wa mto na kuanza kufanya shughuli za kibinadamu ikiwemo kilimo na makazi, jambo ambalo limeongeza athari mto ulipojazwa na mvua za El Nino.

**NI MUHIMU JAMII KUELEWA KWAMBA:**

Bwawa la Mwalimu Nyerere halijachochea mafuriko katika wilaya ya Rufiji, badala yake limepunguza athari za mafuriko. Huenda bila kuwepo kwa bwawa hilo atahri za mafuriko zingekuwa kubwa zaidi ya ilivyo sasa.

Hii ni kwa sababu kabla ya bwawa hilo kujengwa maji yalikuwa yakitiririka kwa kasi na kuleta athari kubwa za mafuriko. Lakini baada ya ujenzi wa bwawa hillo, maji yote ya mto Rufiji yaliingizwa kwenye bwawa na kupunguzwa kasi kabla ya kuachiwa kitaalamu na kwa kasi ndogo kuendelea kutirirka mtoni.

Bwawa la Mwalimu Nyerere lina uwezo wa kufungulia maji mita za ujazo 2,300 tu kwa sekunde. Kiwango hiki hakiwezi kusababisha mafuriko kwa namna yoyote kwa sababu kiwango cha juu cha ujazo mto Rufiji ni Mita za ujazo 13,000 kama ilivyorekodiwa mwaka 1974.

Kuanzia Februari 28, 2024 timu ya TANESCO imepiga kambi katika Wilaya za Rufiji na Kibiti kwa kushirikiana na viongozi mbalimbali wa serikali, kuhamasisha wananchi kuhama katika maeneo hatarishi ikiwemo waliovamia maeneo ya mkondo wa mto.

Hata hivyo Elimu zaidi inapaswa kutolewa kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kutofanya shughuli za kibinadamu katika maeneo ya mkondo wa maji hata kama hakuna maji kwa wkati huo.

# Raia wa Niger waandamana kushinikiza wanajeshi wa Marekani kuondoka



NIAMEY, NIGER

MAMIA ya watu wamefanya maandamano huko Agadez kaskazini mwa Niger, wakitaka kuondoka kwa wanajeshi 1,000 wa Marekani ambao wamekita kambi nchini humo kupambana na wanamgambo wa kijihadi.

Siku mbili zilizopita Washington ilisema imekubali kujiondoa kwao.

Niger ni moja ya nchi kadhaa za magharibi mwa Afrika ambapo viongozi wa kijeshi wamekuwa wakikata uhusiano na washirika wao wa jadi wa magharibi na kuimarisha uhusiano na Urusi.

Watawala wa kijeshi wa Niger wamekuwa madarakani chini ya miezi tisa lakini tayari jeshi la Ufaransa limelazimika kuondoka na wanajeshi wa Marekani watafuata mkondo hivi karibuni.

Washington ilikuwa mshirika wa karibu katika vita dhidi ya wanamgambo wa Kiislamu.

Huku kambi ya ndege zisizo na rubani za Marekani ikikaribia kufungwa, Urusi imekuwa ikitoa msaada kwa wanajeshi na vifaa.

Katika nchi jirani za Mali na Burkina Faso, mapinduzi pia yalifuatiwa na uungwaji mkono wa haraka kuelekea Moscow.

Haya yote yanatokea katika eneo la Afrika Magharibi ambapo wapiganaji wa kijihadi wanasababisha maafa na kuwafurusha mamilioni ya watu kutoka makwao.

# Maafisa wa jeshi la majini la Japan hawajulikani walipo baada ya ajali ya helikopta



TOKYO, JAPAN


AFISA mmoja wa jeshi la majini la Japan amefariki na wengine saba hawajulikani walipo baada ya helikopta mbili kuanguka wakati wa mazoezi ya usiku katika Bahari ya Pasifiki. Mitsubishi SH-60K za injini mbili zilikuwa kwenye mafunzo ya kupambana na manowari karibu na Visiwa vya Izu, kilomita 600 kusini mwa Tokyo, maafisa walisema.

Rekoda mbili za safari za ndege zilipatakana karibu na kila mmoja kama uchafu ikiwa ni pamoja na sehemu za blade za rotor.

Waziri wa Ulinzi Minoru Kihara alisema chanzo cha ajali hiyo hakijajulikana.

"Kwanza tunafanya tuwezavyo kuokoa maisha," Bw Kihara alisema akiongeza kuwa helikopta hizo "zinafanya mazoezi ya kukabiliana na nyambizi usiku". Mwanachama wa wafanyakazi alichukuliwa kutoka kwa maji lakini ilithibitishwa kuwa amekufa.

Mawasiliano na helikopta moja yalipotea saa 22:38 saa za Japan nje ya kisiwa cha Torishima, mtangazaji wa NHK anaripoti.



# TikTok yaonya marufuku ya Marekani 'itaminya uhuru wa kujieleza'

WASHINGTON, MAREKANI

TIKTOK inasema uwezekano wa kupigwa marufuku kwa programu yake nchini Marekani "utaminya uhuru wa kujieleza" wa Wamarekani milioni 170.

Baraza la Wawakilishi la Marekani lilipiga kura Jumamosi kupiga marufuku TikTok ikiwa mmiliki wa programu hiyo hatakatisha uhusiano wake na China.

Sheria hiyo ilikuwa sehemu ya kifurushi cha sera za kigeni za Marekani ambacho kilijumuisha misaada kwa Ukraine na inaweza kuwa sheria mapema wiki ijayo.

Katika miezi ya hivi karibuni maafisa wa Merika wametoa sauti juu ya umaarufu wa TikTok kwa vijana.

Wanadai mmiliki wa TikTok Bytedance yuko chini ya Beijing - mashtaka ambayo imekanusha mara kwa mara.

Sheria ya TikTok ilijumuishwa katika kifurushi, kilichoidhinishwa na wabunge, ambacho kingetuma $61bn (£49bn) kama msaada wa kigeni kwa Ukraine, pamoja na pesa kwa Israeli na Taiwan.

Baraza la Wawakilishi lilipiga kura kuhusu mustakabali wa TikTok kwanza - huku wabunge 360 dhidi ya 58 wakipiga kura kuhusu mswada uliofanyiwa marekebisho wa kuweka au kupiga marufuku.

Bunge la Seneti linatarajiwa kupigia kura mswada huo wiki ijayo na hapo awali Rais wa Marekani Joe Biden alisema kuwa atatia saini sheria hiyo.

Ikiwa mswada huo utakuwa sheria, Bytedance atakuwa na miezi tisa ya kuuza hisa yake - na uwezekano wa kuongezwa kwa miezi mitatu wakati mauzo yanaendelea - au atapigwa marufuku.

# Kwanini CCM imeweza kusalia madarakani kwa miaka yote?

NA EZEKIEL KAMWAGA, BBC

FEBRUARI 5, 2024 chama tawala nchini Tanzania kilitimiza miaka 47 toka kilipozaliwa baada ya kuunganishwa kwa vyama vya TANU na ASP. CCM ni moja ya vyama vichache vya ukombozi ambavyo vimesalia madarakani barani Afrika, je, ipi siri ya mafanikio hayo?

Katika mojawapo ya mahojiano aliyowahi kufanya miaka ya nyuma, Rais Yoweri Museveni wa Uganda alipata kuulizwa anadhani nini hasa ilikuwa siri ya Baba wa Taifa la Tanzania, Julius Nyerere, kudumu muda mrefu madarakani.

Bila kupepesa macho, Rais huyo alitoa jibu moja tu; (aliweza kulidhibiti jeshi). Hilo ndilo jibu lililokuja haraka kichwani kwake na pasi na shaka yoyote, atakuwa amejifunza mengi kiasi kwamba sasa yeye ndiye Rais aliyekaa madarakani kuliko mwingine yeyote miongoni mwa nchi za Afrika Mashariki – akimzidi hata Mwalimu Nyerere aliyekaa miaka 24.

Nyerere alikuwa Rais wa Tanzania lakini hakuwa akiongoza kupitia mapinduzi ya kijeshi. Aliongoza kwanza kupitia chama cha TANU kilichopigania Uhuru wa Tanganyika na baadaye Chama Cha Mapinduzi (CCM) kilichoundwa kufuatia kuungana kwa TANU na Afro Shiraz (ASP) cha Zanzibar mwaka 1977. Kuunganishwa kwa vyama hivi kulitokana na Muungano wa Tanganyika na Zanzibar wa mwaka 1964 na nia ya kuwa na chama kimoja kinachotawala kupitia mfumo huo.



Baada ya kushinda Uchaguzi Mkuu wa 2020, CCM sasa imekaa madarakani kwa miaka 63; na ndicho chama kilichokaa madarakani kwa muda mrefu kuliko kingine chochote miongoni mwa nchi za Afrika.

CCM ni miongoni mwa vyama vichache vya ukombozi ambavyo bado vimesalia madarakani takriban miaka 60 baada ya nchi nyingi za Afrika kuwa huru. Vyama vya aina yake ambavyo bado vimesalia madarakani ni kama FRELIMO cha Msumbiji, SWAPO cha Namibia, MPLA cha Angola, ANC cha Afrika Kusini.

Miongoni mwa hivyo, hakuna ambacho kimekaa madarakani kuizidi CCM.

Washirika wa CCM katika harakati za ukombozi; vyama kama vile UNIP cha Zambia, UPC cha Uganda, KANU cha Kenya na vingine vya Afrika Magharibi na Kaskazini ama vimeondolewa madarakani na kugeuka kuwa vyama vya upinzani vilivyodhoofu au kuondoka kabisa katika ramani za kisiasa.

Nini hasa kimeifanya CCM kudumu muda wote huo wakati wengine wakipotea katika ramani?

**UONGOZI WA JULIUS NYERERE**

Kete ya kwanza ya CCM ni aliyekuwa kiongozi wake kwa takribani miongo mitatu ya kwanza, hayati Mwalimu Nyerere. Rais huyu wa kwanza wa Tanzania alifanya mambo ambayo hatimaye yamesababisha CCM iendelee kubaki madarakani. Yeye ndiye mpishi wa mambo mengine ambayo yamekifanya chama hicho kiwe hapo kilipo sasa.

Wakati rafiki zake, Milton Obote wa Uganda na Kwame Nkrumah wa Ghana wakiondolewa madarakani kwa mapinduzi ya kijeshi, Nyerere alinusurika na tukio la Maasi ya Jeshi ya mwaka 1964. Alichofanya Nyerere ni kulivunja jeshi lililokuwapo ambalo alilirithi kutoka kwa wakoloni na kutengeneza Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ).

Jeshi hilo lilitengenezwa na kufumwa katika itikadi ya ukombozi, ujamaa na lisilo na ukabila, udini huku askari wakipandishwa vyeo kutokana na umahiri wao na si kwa vigezo vingine. Matokeo yake, jeshi hilo la kizalendo halikumsumbua tena kama ambavyo wenzake wengi barani Afrika.

Ni Nyerere ndiye aliyepandisha hadhi lugha ya Kiswahili ambayo iliwaunganisha Watanzania na kuwa lugha ya kisiasa. Kwa sababu hiyo, CCM kikaweza kuwa chama kilichoweza kufika nchi nzima kwa viongozi wake kuzungumza lugha moja inayoeleweka kwa wananchi. Ziko nchi ambazo hata mawasiliano ya vitu vidogo ni ya taabu kwa sababu watu ndani ya serikali, majeshi na kwenye vyama hawazungumzi lugha moja na wakaelewana.

Nyerere hakuwa malaika lakini mtindo wake wa uongozi ulimfanya aheshimiwe na wengi wa Watanzania. Baba huyu wa Taifa hakuwa fisadi, alikuwa mzungumzaji mzuri kwenye majukwaa na kupitia maandishi yake na hakuonekana kuwa na upendeleo wa wazi wazi kwa watu wa dini, kabila au eneo alilotoka.

Nyerere pia ndiye aliyesimika mfumo wa utawala wa Tanzania ambapo Rais anakuwa ni Mkuu wa Nchi, Kiongozi wa Serikali na Amiri Jeshi Mkuu. Haya ni mamlaka makubwa sana kupewa mtu mmoja. Mfumo huu unampa Rais - kiongozi wa chama tawala; CCM tangu Uhuru, madaraka makubwa ya uteuzi wa viongozi wa vyombo vya serikali na dola na chama hicho kimekuwa kikitumia faida hiyo ipasavyo nyakati za uchaguzi.

**KUBADILISHA MARAIS**

Ukiondoa Nyerere, hakuna Rais mwingine wa Tanzania ambaye ametawala kwa zaidi ya miaka kumi. CCM imekuwa na utaratibu wa kuheshimu Katiba ambapo Rais aliye madarakani atatawala kwa miaka kumi tu na kumwachia mwingine.

Katibu Mtendaji wa kwanza wa CCM wakati ilipoanzishwa, Pius Msekwa, alipata kuniambia kwamba viongozi wanaokaa madarakani muda mrefu matokeo yake huchokwa na wananchi wao hata kama hakuna jambo baya walilofanya.

Kwa kuhakikisha wateule wake wanakaa madarakani miaka kumi tu, CCM imehakikisha Watanzania wamekuwa hawachoki kwa kuona sura moja tu kwa miaka zaidi ya kumi. Mara nyingi, mgombea anayechukua nafasi ya aliyetangulia anakuwa na sifa na haiba tofauti na mtangulizi wake.

Nyerere alikuwa mwanafalsafa, mhafidhina na mcheshi, mbadala wake Ali Hassan Mwinyi akawa mtu rahimu, muungwana na mpenda mabadiliko, Mkapa akawa makini na mshaufu huku Jakaya Kikwete akiwa tena mcheshi, mtu wa watu na muungwana wa pwani. Baada ya miaka yake kumi, John Magufuli alichukua nafasi yake naye akawa tofauti na mtangulizi wake kwa haiba na utendaji kazi. Sasa yuko Samia Suluhu Hassan, rais wa

>>Inaendelea Uk. 10



# Kwanini CCM imeweza kusalia madarakani kwa miaka yote?

>>Inatoka Uk. 9

kwanza mwanamke nchini Tanzania, ambaye ni mkweli, makini na mchapa kazi mahiri.

**MGAWANYO WA KEKI YA TAIFA**

Namna pekee ya kuelewa hili ni kuangalia nchi jirani ya Kenya. Wakati nayo ikielekea kutimiza miaka 60 ya Uhuru wake mwaka 2023, imefanikiwa kuwa na marais wanne; Jomo Kenyatta, Daniel Arap Moi, Mwai Kibaki, Uhuru Kenyatta na sasa William Ruto. Hiyo maana yake ni kuwa Wakikuyu wametoa marais watatu na Wakalenjini wametoa marais wawili miongoni mwa marais watano waliowahi kutawala nchi hiyo.

Moi na Ruto si Mkikuyu – wametoka katika kabila la Wakalenjini, ambalo ni la tano kwa ukubwa nchini Kenya nyuma ya Wamasai, Waluhya, Wajaluo na Wakikuyu.

Wakalenjini ni kundi la makabila ya magharibi mwa Kenya, hasa katika Mkoa wa Bonde la Ufa, wanaoongea lugha za Kiniloti zilizo karibu. Wasemaji wa lugha hizo wako pia Tanzania na Uganda.

Kati ya vikundi hivi ni Waelgeyo, Wakipsigis, Wamarakwet, Wanandi, Wasabaot, Waterik na Watugen. Wakati mwingine hata Wapokot wanahesabiwa kati ya Wakalenjini lakini kwa kawaida wanajitazama kama kundi la pekee hata kama lugha yao ni ya karibu.

***Katika nchi ambazo kuna mgawanyo wa madaraka na vyombo vya utoaji haki vinavyojitegemea, si rahisi kusikia Jaji Mkuu mstaafu akijiingiza kwenye uchaguzi kuomba kupitishwa na chama awe mgombea wake urais. Kwa hiyo, CCM imekuwa ikifaidikika na mfumo huu wa kufanya siasa na uchaguzi ulioizunguka.***

Mkoa wa Bonde la Ufa ni mkubwa kati ya mikoa minane ya Kenya. Umepakana na Sudani, Ethiopia, Uganda na Tanzania, halafu na mikoa ya Magharibi, Nyanza, Mashariki, Kati na Pwani. Jina linatokana na Bonde la Ufa linalopita katika mkoa. Eneo la mkoa ni 173,854 km² na makao makuu ya mkoa yapo Nakuru.

Jambo hili limekuwa likizua hali ya sintofahamu na kuhisi kutengwa kwenye mgawo wa keki ya taifa miongoni mwa makabila mengine makubwa nchini humo kama vile Wajaluo, Waluhya, Wakalenjini na watu wa makabila ya Pwani ya Kenya.

Hali ni tofauti kwa Tanzania. Nyerere alikuwa Mzanaki kutoka Kaskazini mwa Tanzania, Mwinyi anatoka Zanzibar, Mkapa anatoka Kusini, Kikwete akatoka Pwani, Magufuli anatoka Kanda ya Ziwa na Samia anatoka Zanzibar.

Marais wote wa Tanzania wametoka katika makabila tofauti miongoni mwa zaidi ya 120 yaliyopo.

Hii maana yake ni kuwa hakuna upande au kabila la Tanzania linaloweza kusema limeongoza kwa kutoa marais wengi. Kitendo cha kuwa na Rais madarakani humaanisha kwamba watu wa eneo analotoka Rais huweza kufaidika kwa namna moja au nyingine na uwepo wa kiongozi miongoni mwao. Inaweza isiwe waziwazi lakini pasi na shaka, kuna kipande cha keki ya taifa kitamegwa kwa kuzingatia ukweli wa Rais kutoka katika eneo fulani.

Uchaguzi mwingine unapofika, kuna wana CCM wataunga mkono mgombea kwa sababu anatoka katika eneo analotoka na hivyo kwamba hata kama haitakuwa kwa kiasi kikubwa; walau wanaweza kujikuta kuambulia kipande kutoka katika Keki ya Taifa.

Kwa upande mwingine, Samia ni mwanamke, hivyo urais wa Tanzania umezingatia pia jinsia na sasa wanawake wanajiona kuwa sehemu ya utawala.

**MWINGILIANO WA DOLA NA CCM**

Ingawa kisheria Tanzania inaongozwa kupitia mfumo wa vyama vingi, mstari mwembamba sana unatenganisha CCM na watendaji wa serikali na vyombo vya dola. Hata vyombo ambavyo kwa kawaida vingetakiwa kutoa haki kwenye washindani wa kisiasa, vinaonekana kuwa na uhusiano na CCM.

Katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, aliyewahi kuwa Jaji Mkuu wa Tanzania, Augustino Ramadhani, alijitokeza kutaka kuwania Urais kupitia CCM.

Mwaka 2020, aliyekuwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC), Jecha Salum Jecha, alitangaza nia ya kutaka apitishwe na CCM kuwania urais wa Tanzania. Nchini Tanzania, watumishi kama wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya wanatakiwa kuwa watumishi wa umma lakini vyeo vyao hivyo vya kiserikali vinawapa fursa ya kuingia kwenye vikao vya CCM kwa mujibu wa nyadhifa zao.

Inapofika nyakati za uchaguzi, ofisi hizi za umma kimsingi hubadilika na kugeuka za CCM kwa maana ya matumizi ya rasilimali watu na nyingine.

Katika nchi ambazo kuna mgawanyo wa madaraka na vyombo vya utoaji haki vinavyojitegemea, si rahisi kusikia Jaji Mkuu mstaafu akijiingiza kwenye uchaguzi kuomba kupitishwa na chama awe mgombea wake urais.

Kwa hiyo, CCM imekuwa ikifaidikika na mfumo huu wa kufanya siasa na uchaguzi ulioizunguka.

**SUALA LA KATIBA**

Katiba ya Tanzania ilitengenezwa mwaka 1977; nyakati zilezile wakati CCM ikiundwa. Katiba hii ndiyo inampa Rais mamlaka na madaraka aliyonayo ikiwamo kuteua viongozi wa taasisi zinazosimamia uchaguzi.

Wakati wa utawala wa Rais Kikwete, Tume ya Marekebisho ya Katiba iliyoongozwa na Waziri Mkuu mstaafu, Joseph Warioba, ilikusanya maoni ya Watanzania wote kuhusu Katiba mpya na ilipendekeza mambo ya kubadili kwenye Katiba ili kuongeza uwajibikaji na kupunguza madaraka ya Rais yaliyomo katika Katiba ya sasa.

Hata hivyo, mapendekezo hayo yalipingwa na wabunge wa Bunge la Katiba waliokuwa upande wa chama tawala kwa vile ilionekana kama inataka kupunguza madaraka na mamlaka ya Rais. Matokeo yake ni kwamba Watanzania wamebaki na Katiba ileile ya mwaka 1977 iliyotungwa wakati chama kikiwa kimeshika hatamu.

Afrika Kusini, Kenya, Malawi na Zambia wamefanya mabadiliko ya Katiba zao wakati wakienda kwenye chaguzi zao na matokeo yake yakawa mazuri kwa wapinzani. CCM, pamoja na mambo mengine, inaendelea kubaki madarakani kwa sababu Katiba iliyopo ilitungwa kwa lengo la kuisimika ibaki madarakani milele.

Ndiyo sababu, kuna wanaoamini kwamba kama vyama vya upinzani vina lengo kweli la kuing'oa CCM madarakani, sehemu ya kwanza wanayotakiwa kuipigania ni kuhakikisha kunakuwa na mabadiliko ya Katiba ya Tanzania inayotumika sasa.



# Umuhimu wa chakula katika shule za awali

NA SAMWEL MWANGA, SIMIYU

SHULE ya awali ni kituo cha kuwalelea au kuwasomesha watoto wadogo ambao hawajaanza elimu ya msingi (darasa la kwanza) na kwa sasa serikali imeagiza kwa shule zote za msingi zinazomilikiwa na serikali zimetakiwa kuwa na madarasa ya wanafunzi wa Awali.

Na kwa msingi huo hata miundo mipya ya idara za serikali katika halmashauri za wilaya ambazo ndizo ziko karibu wa wananchi kumeanzishwa Divisheni ya Elimu ya Awali na Msingi.

Katika vituo vya shule ya awali, mara nyingi watoto huwa na umri kati ya miaka 2 mpaka 6 au zaidi kidogo. Umri huo ni muhimu sana kwa maendeleo ya mtoto, kimwili na kiroho.

Chakula kina nafasi kubwa ya kumjenga mtoto kimwili na wengine wanasema hata kiroho. Kwa hiyo, umuhimu wa chakula katika vituo hivyo ni jambo lililowazi.

Hata hivyo, kwa vile bado kuna baadhi ya shule za awali hasa wazazi ambao wanaona kuwa suala la chakula katika vituo vyao si muhimu na litaongeza gharama.

Lakini ni lazima jamii izinduliwe hasa wazazi wa aina hiyo kwa kuielimisha jamii kwa ujumla juu ya dhana ya chakula katika shule ya awali.

"Kuna Wazazi bado wanaona chakula kwa wanafunzi wa awali kuwa ni gharama hivyo wanapaswa kuelimishwa juu ya umuhimu wa chakula kwa wanafunzi hao katika kujifunza sambamba na makuzi yao," amesema Mwl Rose Joseph wa Shule ya Awali kanisa la Anglikana wilaya ya Maswa.

> **_Katika kutayarisha chakula cha watoto wa shule ya awali, mwalimu au mlezi lazima azingatie mafungu makuu ya chakula ambayo ni chakula cha kujenga mwili, chakula cha kuupa mwili nguvu na joto pamoja na chakula cha kulinda mwili,"_**

Amesema tunacho kula kina faida kubwa moja, nayo ni kutupatia virutubisho (nutrients) hivyo virutubisho vina kazi kubwa tatu mwilini.

Mwl Rose anazitaja kazi hizo huku akibainisha ya kuwa kazi ya kwanza ni kujenga mwili huku akitolea mfano kuwa watu wote tuna jua kuwa binadamu kwa hali ya kawaida huzaliwa na baba na mama.

Anasema anapozaliwa huwa ni mdogo na hapo tunamwita mtoto mchanga. Baada ya miaka kadhaa huwa mkubwa na kuweza kufanya mambo yake mwenyewe. Mwanaadamu kama huyo anaweza kuongezeka umbo, kutoka mtoto na kuwa mkubwa kwa sababu ya virutubisho vinavyotokana na vyakula tunavyokula.

Kazi ya pili ya virutubisho ni kuupa mwili nguvu na joto. Mambo au kazi mbalimbali zinazofanywa na binaadamu zinawezeshwa na nguvu (energy) inayotokana na virutubisho. Kutembea, kuongea, kulia, kubeba mizigo, kusoma, n.k. ni baadhi tu ya kazi hizo.

Kazi ya tatu ya virutubisho ni kulinda mwili usipate magonjwa.

"Ulaji duni na magonjwa ni sababu kubwa zinazosababisha vifo vingi kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano katika nchi hasa za ulimwengu wa tatu ikiwemo Tanzania,"amesema.

Mwl Rose anasema kuwa taarifa ya shirika la Umoja wa Mataifa.

linalojishughulisha na mambo ya watoto (UNICEF) ya mwaka 1990 inaonyesha kuwa watoto 176 kati ya watoto 1000 wanaozaliwa Tanzania hufa kila mwaka kabla ya kutimiza umri wa miaka mitano.

Naye Mkuu wa Divisheni ya Shule za Awali na Msingi,Mwl Lucy Kulongwa amesema kuwa ni muhimu watoto katika shule ya awali (madarasa, chekechea) wapatiwe chakula cha kutosha, safi na salama na kilicho mlo kamili (balanced diet).

Amesema hii ni kwa sababu baadhi yao wanatoka nyumbani bila kula chakula chochote na wengine wanakaa mbali, wanapoteza muda mwingi njiani kabla ya kufika nyumbani.

"Katika kutayarisha chakula cha watoto wa shule ya awali, mwalimu au mlezi lazima azingatie mafungu makuu ya chakula ambayo ni chakula cha kujenga mwili, chakula cha kuupa mwili nguvu na joto pamoja na chakula cha kulinda mwili,"amesema.

Amesema chakula cha kujenga mwili ni muhimu sana kwa watoto wa shule ya awali. Hii ni kwa sababu mwili wake (pamoja na akili) unahitaji kujengeka na kukua.

Mwl Kulongwa amessma vyakula vinavyojenga mwili ni kama vile maziwa, nyama, samaki, mayai, senene, ndege, maharage, choroko, soya, njegere na karanga

Pia amesema kuwa watoto hufanya shughuli mbalimbali kama vile kucheza, kusoma, kukimbia, n.k. ili mwili uweze kumudu kazi hizo na zile za kujenga mwili, lazima mwili upate vyakula vyenye kutoa nguvu huku akivitaja vyakula hivyo kuwa ni mchele, viazi, mahindi, mtama, ndizi, karanga, alizeti, samli, siagi, asali na mihogo hivyo vyote kuupa mwili nguvu na joto.

Amesema vyakula vya kulinda mwili hivi husaidia kulinda mwili wa mtoto asipatwe na magonjwa mbalimbali huku akitolea mfano wa vyakula hivyo ni kama vile mbogaamboga (mboga za majani, nyanya, karoti) na matunda mbalimbali, embe, machungwa, mananasi, papai, ubuyu, ukwaju )

"Zaidi ya makundi hayo ya vyakula, watoto wa shule za awali lazima wapatiwe maji safi na salama yaliyochemshwa na kuchunjwa na kuhifadhiwa katika chombo safi,"Amesema.

Hivyo ni matarajio makubwa kwa wamiliki wa shule hizi za awali hasa zilizo nyingi zinamilikiwa na watu binafsi wakiwemo wazazi na jamii kwa ujumla wataendelea kutoa chakula bora na maji safi na salama kwa watoto wetu na wale ambao bado hawajaanza kutoa huduma hiyo wataanza sasa la sivyo tuaathiri ukuaji wa watoto hao.



TPA TANZANIA PORTS AUTHORITY
MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BANDARI TANZANIA






> Ipo miradi ya kimkakati inatarajia kuzalisha sehemu ya ajira hizi, ikiwemo ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Msalato, Uwanja wa Mpira Dodoma, Ujenzi wa Bomba la Mafuta kutoka Uganda sambamba na ajira za moja kwa moja serikalini.

# Uwekezaji Bandari na mkakati wa ajira milioni nane za Samia

NA MWANDISHI WETU, KISARAWE

UWEKEZAJI wa kampuni ya DP World ya Dubai kwenye Bandari ya Dar es Salaam unatarajiwa kuzalisha takriban ajira mpya 42,917, idadi ambayo itafanya kuongezeka kwa ajira kutoka 28,990 za sasa hadi ajira 71,907. Ongezeko hili linaleta matumaini makubwa ya namna Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, inavyojitahidi kupambana na changamoto ya ukosefu wa ajira, ambayo imezikumba nchi nyingi duniani.

Wakati ambapo mataifa makubwa ulimwenguni yanawaza kupunguza ajira za mamilioni ya watu kwa kutumia teknolojia ya akili bandia (AI), Rais Samia anatafuta fursa mpya za ajira katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM). Itakumbukwa kwamba, Ripoti ya benki ya uwekezaji ya Goldman Sachs, ilisema kwamba, teknolojia ya akili bandia inaweza kuchukua nafasi za kazi za kudumu saa na milioni 300.

Ikaelezwa kwamba, AI inaweza kuchukua nafasi karibu robo ya kazi nchini Marekani na bara lote la Ulaya lakini inaweza kumaanisha pia kutengeneza nafasi mpya za kazi na kuongeza tija pamoja na kuongeza thamani ya bidhaa na huduma kwa kila mwaka zinazozalishwa duniani kote kwa 7%.

Ripoti hiyo ikasema, akili bandia ya uzalishaji, yenye uwezo wa kuunda maudhui yasiyoweza kutofautishwa na kazi ya binadamu, ni "maendeleo makubwa". Kwa upande mwingine, Serikali ya Uingereza ina nia ya kuongeza uwekezaji katika teknolojia ya akili bandia, ambayo inasema "hatimaye italeta tija katika uchumi wote", na imejaribu kuwahakikishia umma kuhusu athari zake.Kitu pekee ambacho hakijulikani ni kwamba hakuna njia ya kujua ni kazi ngapi zitaathiriwa na zitafanywa na akili bandia (AI) ya uzalishaji.

Waandishi wa habari watakabiliwa na ushindani zaidi, ambao unaweza kupunguza mishahara yao, vinginevyo labda kuwe na ongezeko kubwa la mahitaji ya kazi hiyo.

Kwa mujibu wa utafiti uliotajwa na ripoti hiyo, asilimia 60% ya wafanyakazi wako kwenye kazi ambazo hazikuwepo mwaka 1940.

Lakini utafiti mwingine unaeleza kuwa mabadiliko ya kiteknolojia tangu miaka ya 1980 yamewahamisha wafanyakazi kwa kasi zaidi kuliko ilivyozalisha ajira. Na ikiwa AI ya uzalishaji ni kama maendeleo ya awali ya teknolojia ya habari, ripoti hiyo inahitimisha kuwa, inaweza kupunguza ajira katika muda mfupi ujao.

## JITIHADA ZA RAIS SAMIA

Wakati mabadiliko hayo yanafikiriwa kufanyika kwenye mataifa makubwa kabla ya kusambaa kwenye nchi zinazoendelea, Rais Samia na chama chake cha CCM wanafikiria namna ya kutengeneza ajira mpya kwa vijana na wanawake ili kukuza uchumi.

Hatua ya kuruhusu uwekezaji kwenye Bandari inamaanisha kwamba, kuna fursa nyingi zitakazopatikana, kuanzia ajira za kudumu hadi za muda mfupi.

Kwa mfano, ukiacha ajira hizo 43,000 zitakazozalishwa kwenye sekta hiyo, bado ziko fursa nyingine nyingi kwa jamii kupata ajira.

Fikiria ni ajira ngapi zitakazozalishwa wakati Zambia itakapoanza kujenga Bandari Kavu katika eneo la Kwala wilayani Chalinze baada ya Rais Samia kuipatia nchi hiyo jumla ya hekta 20 (ekari 50).

Zambia ni miongoni mwa nchi zinazoitegemea Bandari ya Dar es Salaam kusafirisha shehena yake – iwe kutoka ama kwenda ng'ambo – hivyo kuwa na Bandari Kavu maana yake itaondoa usumbufu wa namna ya kuhifadhi mizigo yao kabla ya kusafirisha.

Kwa mujibu wa taarifa kutka serikalini, nchi nyingine kama Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Burundi, Malawi na Rwanda zitapewa heka 10 (ekari 25) kila moja kwenye eneo la Bandari Kavu ya Kwala ili kuhifadhi mizigo yao.

Na kwa kuongeza ufanisi wa Bandari ya Dar ess Salaam baada ya uwekezaji wa DP World, maana yake ni kwamba, kutakuwepo na mizigo mingi ambayo inaweza kutoka kwa wakati mmoja bandarini lakini ikahitaji kuhifadhiwa kabla ya kusafirishwa, kwa sababu kuisafirisha kwa wakati mmoja nako kunaweza kuwa changamoto hata kama miundombinu inaruhusu.

Kwahiyo hapa unazungumzia ajira kwenye kampuni za wakandarasi watakaojenga, ambao watahitaji vibarua wa moja kwa moja, lakini pia wanajamii wa maeneo ya karibu watapata ajira nyingi ndogo ndogo, zikiwemo hata za mama na baba lishe, uuzaji wa nafaka pamoja na wanyama na ndege (ng'ombe, mbuzi na kuku) kwa ajili ya kitoweo, na kadhalika.

Ndiyo. Juzi Jumanne, Oktoba 24, 2023, Rais Samia akihutubia Sherehe za Miaka 59 ya Uhuru wa Zambia katika Ikulu ya Lusaka ambako alikuwa mgeni rasmi, alitoa zawadi kwa Zambia ya hekta 20 katika eneo la Kwala mkoani Pwani, kwa ajili ya kurahisisha uchukuaji wa mizigo bandarini.

Pamoja na hayo, Rais Samia akasema Tanzania imetengeneza mazingira mazuri ya ushirikiano na Zambia katika maeneo zaidi ya sita ikiwemo biashara, miundombinu na kujenga bomba la gesi kutoka Tanzania hadi Zambia. Maeneo mengine aliyotaja ni kwa pamoja nchi hizo kuhamasisha amani katika nchi za Afrika na Dunia kwa ujumla na kuendeleza miradi iliyopo ukiwemo wa Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (Tazara).

Alisema kupitia mipango ya Tanzania ya kurahisisha zaidi biashara kati ya nchi hizo mbili, serikali imetenga eneo hilo la Bandari Kavu ya Kwala mkoani Pwani kwa ajili ya mizigo inayopelekwa Zambia.

"Zaidi ya hayo, Zambia itawezeshwa kwa muda mrefu zaidi wa kuhifadhi bila malipo mzigo ambao unaenda hadi siku 45. Hatua hii itapunguza msongamano na ucheleweshaji, na hatimaye kupunguza gharama za kufanya biashara nchini Zambia," alisema na kuongeza kwamba, hatua hiyo inatarajia kukuza biashara kati ya nchi hizo mbili na kutengeneza fursa zaidi za kibiashara kwa wananchi wa pande zote mbili. "Hii ni zawadi kutoka Tanzania unaposherehekea uhuru wako," alisema Rais Samia na kushangiliwa na wananchi wa Zambia.

Akasema, Serikali yake imeanza uboreshaji wa mitambo ya Bandari ya Dar es Salaam ili kuhakikisha bandari hiyo inafanya kazi kwa ufanisi, kwa wakati na bila vikwazo katika shughuli zake. "Ningependa kutoa wito kwa jumuiya ya wafanyabiashara nchini Zambia kuchangamkia fursa hii ya kipekee," alisema.

Kwahiyo basi, fursa hii ya Bandari Kavu ya Zambia pale Kwala inamaanisha kwamba ajira zaidi zitazalishwa, ikiwemo kwenye sekta nzima ya usafirishaji. Hapo bado hujazungumzia kuhusu nchi nyingine kama Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Malawi, Burundi na Rwanda ambazo nazo zinaitegemea Bandari ya Dar es Salaam kusafirisha shehena zao za mizigo.

## SEHEMU YA AJIRA MILIONI 8

Uzalishaji wa fursa hizi za ajira ni sehemu ya mkakati wa Serikali ya Awamu ya Sita ambapo Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2020-2025 imeahidi kwamba, Serikali itazalisha ajira zaidi ya milioni nane katika sekta rasmi na isiyo rasmi hadi kufikia mwaka 2025.

Ipo miradi ya kimkakati inatarajia kuzalisha sehemu ya ajira hizi, ikiwemo ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Msalato, Uwanja wa Mpira Dodoma, Ujenzi wa Bomba la Mafuta kutoka Uganda sambamba na ajira za moja kwa moja serikalini.

Sekta ya kilimo itaendelea kuongoza katika kutoa ajira ikifuatiwa na Ofisi ya Rais (Tamisemi), Ofisi ya Waziri Mkuu, Afya, Utumishi wa Umma, Uvuvi, Madini, Viwanda na Biashara na Maliasili na Utalii. Hii inatokana na ukweli kwamba, ukuaji wa uchumi wa viwanda unategemea zaidi malighafi za kilimo, ambapo wananchi wengi wataendelea kujikita kwenye sekta hiyo kuongeza uzalishaji wa mazao yanayohitaji kuchakatwa.

Takwimu zilizopo zinaonyesha kwamba, utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika kipindi cha kuanzia 2016/17 hadi robo ya pili ya 2019/20 ulizalisha jumla ya ajira 12,602,526, ambapo kati ya hizo ajira 11,721,172 zilikuwa za moja kwa moja na ajira 881,354 zisizo za moja kwa moja.

Sekta ya kilimo ndiyo iliyoongoza kwa kuzalisha ajira 4,968,859 za moja kwa moja, ikifuatiwa na Tamisemi (ajira 2,473,647), Ofisi ya Waziri Mkuu (1,823,106), Afya (1,283,407), Utumishi wa Umma na Utawala Bora (627,676), Uvuvi (535,473 zikiwemo ajira 500,000 za muda), Madini (332,468), Mawasiliano (192,069), Ujenzi (104,844), Viwanda na Biashara (86,246), Maliasili na Utalii (61,296), Mifugo (36,238) na Uchukuzi (24,611).

Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa mwaka 2020-2025 imeainisha vipaumbele sita vikuu.

Vipaumbele hivyo vikuu kwenye Ilani ni; Kulina nda kuimarisha misingi ya heshima, usawa, haki na utawala bora ili kudumisha amani, umoja na mshikamano wa taifa; Kukuza uchumi wa kisasa, mshikamano, jumuishi na shindani unaojengwa juu ya msingi wa viwanda, huduma za kiuchumi na miundombinu wezeshi; Kubadilisha kilimo, mifugo na uvuvi ili kuhakikisha usalama wa chakula na usalama wa chakula wakati wote na kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya kiuchumi. Nyingine ni; Kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za afya, elimu, maji, umeme na makazi vijijini na mijini; Kuchochea matumizi ya utafiti, sayansi, teknolojia na uvumbuzi kama nyenzo ya maendeleo ya haraka ya kijamii na kiuchumi; na Kutengeneza ajira zisizopungua 8,000,000 (milioni nane) katika sekta rasmi na isiyo rasmi kwa vijana.

Katika kukuza uchumi, Ilani hiyo inaeleza kuwa Serikali itaendelea kujenga na kukuza uchumi shindani hasa kupitia sekta za huduma za viwanda na uchumi zitakazowezesha ustawi wa wananchi wote. Aidha, itaendelea kuimarisha miundombinu ya kimkakati ili kuweka mazingira wezeshi kwa wananchi kufanya shughuli zao kwa ufanisi; kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kukua na kustawi pamoja na kuvutia wawekezaji kutoa mchango wa maana katika maendeleo ya nchi.

Serikali pia imedhamiria kuleta mageuzi ya kilimo, mifugo na uvuvi ili kuhakikisha usalama wa chakula wakati wote na kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya kiuchumi. Kwa msingi huo, mikakati iliyopo ni kuhakikisha tija inaongezeka katika uzalishaji wa chakula, mifugo na uvuvi kwa ajili ya usalama wa chakula na lishe; Kuongeza tija katika kilimo, mifugo na uvuvi kwa ajili ya kuchochea maendeleo ya kiuchumi hasa katika sekta ya viwanda na huduma; Kuimarisha ushirikiano ili kuongeza nguvu ya wazalishaji hasa katika kupata pembejeo na kutafuta masoko ya ndani na nje ya nchi; Kwa upande wa ajira, Serikali ina mpango wa kuchochea ukuaji wa uchumi hasa katika sekta ya viwanda vinavyotumia malighafi za kilimo, mifugo, uvuvi, madini, maliasili na sekta ya huduma za kiuchumi ikiwemo utalii.

Serikali ina mpango wa kuwawezesha vijana kushiriki katika shughuli za ujasiriamali ikiwa ni pamoja na kuwapatia mafunzo na kuwaunganisha na taasisi na taasisi za mikopo yenye riba nafuu na kuhakikisha miradi mikubwa ya kimkakati inaajiri vijana wengi wa Kitanzania.

Miradi mingi ya kimkakati inayotekelezwa imeendelea kutengeneza ajira nyingi kwa Watanzania, hasa vijana na wanawake, zikiwemo za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja.

Kwa mfano, Mradi wa Umeme wa Maji wa Julius Nyerere (JNHPP-MW2115) katika Bonde la Mto Rufiji, umeajiri zaidi ya vijana 4,000 wa Kitanzania kutoka maeneo mbalimbali nchini, ikiwa ni pamoja na kuzunguka eneo la mradi.

Aidha, mradi huo utakapofikia kilele, utaajiri zaidi ya Watanzania 6,000 na hivyo kuongeza ajira zisizo za moja kwa moja mfano chakula, malazi na mengineyo. Hadi sasa wananchi wa Kijiji cha Kisaki kilichopo kilomita 60 kutoka eneo la mradi wamenufaika na mradi huo kwa kutafuta fursa za kufanya biashara na kukuza uchumi. Ujenzi wa nyumba bora za kulala wageni pia umeongezeka Kisaki huku bei ya ardhi ikiongezeka maradufu.

Ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) pia umetoa ajira 18,000 kwa vijana wa Kitanzania hasa vijana wanaohusika moja kwa moja na mradi huo huku maelfu ya wengine wakinufaika kwa kufanya biashara kando ya mradi huo.

Utekelezaji wa Kanda Maalum ya Kiuchumi ya Bagamoyo (BSEZ) unatoa fursa ya ujenzi wa viwanda takriban 190 na baadaye 790, hatua ambayo siyo tu itaongeza ajira, bali kukuza uchumi wa Taifa kupitia ukusanyaji wa kodi za Serikali.

Kwa mujibu wa taarifa zilizopo, awamu ya kwanza ya mradi wa Bagamoyo SEZ itazalisha ajira 20,000 za moja kwa moja, ambapo mapato ya kodi ya Pay As You Earn (PAYE) yatakuwa makubwa kwa serikali kutoka eneo hilo hilo.

Wakati wa uzinduzi wa kampeni Program ya Jenga Kesho iliyo Bora (BBT) inayowahusisha vijana na wanawake, Rais Samia alisema program hiyo inatarajia kuzalisha ajira milioni 3.

Awamu ya kwanza ya program ya BBT imeshuhudia jumla ya vijana 812 - kati yao wanawake 282 sawa na asilimia 34.73 na wanaume 530 sawa na asilimia 65.27 - wakichaguliwa kujiunga na mafunzo na sasa wamepatiwa mitaji na maeneo ya kufanyia kilimo biashara kupitia mashamba ya pamoja (block farms).




Vijana hao walipatiwa mafunzo kwa kipindi cha miezi minne katika vituo 15 vilivyoandaliwa, ambapo Serikali iligharamia malazi, chakula na gharama za mafunzo.

Kwa maana hiyo, uwekezaji wa Bandari umekuja na fursa nyingi za ajira ambazo zinapita katika mkondo ule ule wa kuhakikisha azma ya Serikali ya Awamu ya Sita kuzalisha ajira milioni 8 kufikia mwaka 2025 inatimia.



TPA TANZANIA PORTS AUTHORITY
MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BANDARI TANZANIA



# Faida kuu 10 za kunyonyesha mtoto



NA MASHIRIKA YA HABARI

KUNYONYESHA kuna manufaa kwa mtoto na mama. Mtaalamu wetu wa lishe aliyeidhinishwa huchunguza manufaa ya kunyonyesha, pamoja na chaguo kwa wale ambao hawawezi kufanya hivyo.

**KUNYONYESHA NI NINI?**

Neno "kunyonyesha" linamaanisha kitendo cha mama kumnyonyesha mtoto wake kwa maziwa ya mama, kwa kawaida moja kwa moja kutoka kwa titi. Nchini Uingereza, akina mama wanashauriwa kunyonyesha maziwa ya mama pekee kwa miezi sita ya kwanza ya maisha ya mtoto wao, na kuendelea kwa muda wanaotaka, huku wakianzisha mlo wa aina mbalimbali hatua kwa hatua.

**FAIDA 10 KUU ZA KUNYONYESHA**

Maziwa ya mama huchukuliwa kuwa lishe bora kwa mtoto wako.

Rahisi kusaga na kuwapa virutubishi vingi watoto wanavyohitaji katika miezi sita ya kwanza, ina faida nyingi za kiafya. Kunyonyesha sio tu husaidia kujenga uhusiano kati ya mama na mtoto, lakini pia ni manufaa kwa afya ya mama.

Kwa watoto wachanga:

Hutoa viungo muhimu kwa maendeleo ya afya,

Ina virutubisho bora kwa mtoto anayekua, Hutoa kile kinaitwa pre na probiotics, Inaweza kusaidia kulinda dhidi ya magonjwa, Husaidia kuzuia fetma ya utotoni, na Inaweza kuongeza uwezo wa ubongo. Kwa akina mama:

Husaidia kudhibiti uzito,

Huboresha ahueni baada ya kujifungua, Inaweza Kupunguza Hatari ya saratani na magonjwa mengine, na Inaweza Kusaidia Kupambana na msongo wa mawazo.

**KUNA FAIDA GANI ZITOKANAZO NA KUNYONYESHA MTOTO WAKO?**

1. Hutoa viungo muhimu kwa maendeleo ya afya - Maziwa ya kwanza, yaitwayo kolostramu, yana protini nyingi, sukari kidogo na yamejaa kingamwili na sababu za ukuaji. Maziwa haya ni muhimu hasa kwa sababu yameundwa ili kukuza maendeleo ya njia ya utumbo wa mtoto, ambayo huimarisha uwezo wake wa kupambana na maambukizi ya bakteria na virusi.

Kolostramu imesheheni kingamwili za mama na immunoglobulin A (IgA). Mwisho ni sehemu muhimu ya mfumo wa kinga, ambayo hufanya safu ya ulinzi katika njia ya kupumua na utumbo wa mtoto.

2. Ina virutubisho bora kwa mtoto anayekua - Kutoa karibu kila kitu ambacho mtoto anahitaji kwa miezi sita ya kwanza ya maisha, maziwa ya mama yana protini nyingi, vitamini, mafuta na sukari.

Maziwa ya mama yanaendana na ukuaji wa mtoto na mabadiliko ya mahitaji ya lishe. Hiyo ilisema, kuna kirutubisho ambacho ulaji wake unaweza kuwa mdogo kuliko inavyotakiwa: vitamini D.

Nchini Uingereza, Idara ya Afya inapendekeza kwamba wanawake wajawazito na wanaonyonyesha watumie kirutubisho cha 10 mcg cha vitamini D, na watoto wanaonyonyeshwa maziwa ya mama pekee wapate kirutubisho cha kila siku cha 8.5 hadi 10 mcg ya vitamini D. vitamini D.

Hii ni kwa sababu idadi ya watu wa Uingereza huelekea kuwa na upungufu wa vitamini D, haswa kati ya makabila fulani.

Vyanzo vya chakula, ambavyo ni pamoja na samaki wa mafuta na viini vya mayai, ni mdogo, na vitamini D nyingi huzalishwa na hatua ya jua kwenye ngozi yetu.

3. Hutoa pre na probiotics - Mbali na virutubisho kwa mtoto, maziwa ya mama yana bakteria yenye manufaa inayoitwa probiotics, pamoja na mafuta ambayo bakteria hawa wanahitaji kukua, inayoitwa prebiotics.

Probiotics zote mbili na prebiotics huchangia katika uanzishwaji wa utumbo wenye afya. Ujuzi wetu katika eneo hili unakua na inakuwa wazi kuwa utumbo wenye afya una jukumu muhimu katika afya yetu ya muda mrefu.

Uchunguzi unaonyesha kuwa kujaza matumbo na bakteria ya probiotic katika hatua hii ya mapema ya maisha kunaweza kusaidia kupunguza matukio ya hali ya atopiki, pamoja na pumu.

4. Inaweza kusaidia kinga dhidi ya magonjwa - Kunyonyesha kunaweza kusaidia kupunguza hatari ya magonjwa kadhaa, ikiwa ni pamoja na ugonjwa wa celiac na eczema ya atopiki, pamoja na maambukizi ya sikio, ugonjwa wa tumbo, ugonjwa wa kifo cha ghafla cha watoto wachanga na leukemia. Zaidi ya hayo, kunyonyesha kwa muda mrefu kunaweza kumlinda mtoto wako akiwa mtu mzima dhidi ya magonjwa kama vile kisukari cha aina 1 na ugonjwa wa moyo.

5. Husaidia kuzuia unene wa kupindukia ututoni - Kunyonyesha kunakuza uzito mzuri na husaidia kuzuia unene wa utotoni. Wataalamu wanaamini kuwa hii inaweza kuwa kutokana na jinsi unyonyeshaji unavyoathiri mimea yenye afya ya utumbo.

Kuchelewesha kuachisha kunyonya hadi umri wa miezi sita kunaweza kuimarisha manufaa haya kwa siku zijazo.

Kwa kupendeza, vyakula ambavyo mama hula wakati wa kunyonyesha vinaweza kuathiri mapendeleo ya ladha ya mtoto wake wakati wa kuachishwa kunyonya na zaidi. Wanawake wanaojifanyia uchaguzi bora wanaweza kuweka msingi wa maisha bora ya baadaye kwa mtoto wao.

6. Inaweza kuongeza uwezo wa ubongo - Kunyonyesha kunaweza kusaidia hata ukuaji wa ubongo wa mtoto, haswa ikiwa wamezaliwa mapema. - Uchunguzi unaonyesha kwamba watoto wanaonyonyeshwa wana alama ya juu ya akili na wana uwezekano mdogo wa kuendeleza matatizo ya tabia na kujifunza.

7. Husaidia kudhibiti uzito - Katika kipindi cha miezi mitatu ya kwanza baada ya kujifungua, mahitaji ya nishati na hamu ya kula ya mwanamke huongezeka, huku baadhi ya wanawake wakihifadhi mafuta ili kukabiliana na uzalishwaji wa maziwa.

Baada ya miezi michache ya kwanza, wanawake wengi hupungua uzito kwani uchomaji wa mafuta huanza kuongezeka, kushuka kwa kilo 0.5 hadi 1 kwa mwezi.

8. Huboresha ahueni baada ya kujifungua - Kunyonyesha kunakuza kutolewa kwa homoni ya oxytocin, ambayo husaidia kupunguza upotezaji wa damu baada ya kuzaa na kurudisha nyumba ya mtoto katika saizi yake ya kabla ya ujauzito.

9. Inaweza kupunguza hatari ya kansa na magonjwa mengine - Kunyonyesha kunaweza kupunguza hatari ya magonjwa kadhaa, pamoja na saratani ya matiti, saratani ya ovari na kisukari cha aina ya 2.

Kunyonyesha kwa zaidi ya mwaka, wakati wa maisha ya uzazi wa mwanamke, kunahusishwa na kupunguza 28% ya hatari ya saratani ya matiti na ovari. Wanawake wanaonyonyesha pia wanaweza kufaidika kutokana na hatari ndogo ya shinikizo la damu na ugonjwa wa moyo.

10. Inaweza kusaidia kushinda msongo wa mawazo - Uchunguzi unaonyesha kuwa kunyonyesha kunaweza kupunguza hatari ya unyogovu baada ya kuzaa.

Hali hii huathiri hadi asilimia 15 ya mama wachanga. Maelezo moja ni kwamba kunyonyesha kunakuza kutolewa kwa oxytocin, homoni ambayo inakuza utulivu, hupunguza mkazo na kukuza hali.

**JE, KUNYONYESHA KUNAFAA KWA KILA MTU?**

Ni muhimu kukumbuka kuwa kila mama na mtoto ni wa kipekee na kunyonyesha sio sawa kwa kila mtu. Akina mama wengi huamua kunyonyesha, lakini ukweli ni kwamba wengi wataishia kutumia mchanganyiko. Ikiwa huwezi kunyonyesha au kuamua kutonyonyesha, fomula itatoa virutubisho vyote anavyohitaji mtoto wako, ikiwa ni pamoja na vitamini D.

Huko Uingereza, muundo wa fomula ya watoto unadhibitiwa kabisa, ingawa viungo vinaweza kutofautiana kidogo kati ya chapa.

Ikiwa haunyonyeshi lakini mtoto wako alizaliwa kwa uke, unaweza kuhakikishiwa kwamba microbiota ya mtoto wako, bakteria hizo zenye manufaa ambazo zina jukumu muhimu katika afya kwa ujumla, zitakuwa zimefaidika kutokana na uhamisho wa bakteria yako mwenyewe wakati wa kujifungua.

Hatimaye, ni vizuri kukumbuka kwamba kiasi chochote cha maziwa ya mama kina athari nzuri.

Kwa hivyo hata kama ungeweza kunyonyesha kwa muda mfupi tu, utakuwa tayari umefanya mabadiliko chanya kwa mustakabali wa mtoto wako. Ikiwa una wasiwasi wowote, zungumza na mkunga wako, au muuguzi.

# UWT Njombe: Rais Samia kielelezo cha misingi ya uongozi, utawala bora

NA MWANDISHI WETU

MIAKA mitatu ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan inaendelea kuzungumzwa kwa namna tofauti kutokana na mageuzi aliyoyafanya katika nyanja mbalimbali.

Rais Samia ambaye ni mwanamke wa kwanza kushika nafasi hiyo ya juu nchini alitimiza miaka mitatu Machi 19 mwaka huu tangu alipoapishwa kurithi nafasi ya Dk. John Magufuli.

Tangu wiki iliyopita kumekuwa na taarifa mbalimbali kupitia vyombo vya habari, mitandao ya kijamii, viongozi, taasisi na mtu mmoja mmoja zikiangazia miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia.

Kubwa linalozungumzwa ni hatua ambayo imepigwa na Rais Samia tangu alipochukua kijiti cha kuiongoza Tanzania mpaka sasa.

Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Njombe, Scholastika Kevela, anaeleza uimara uliofanywa na Rais Samia ndani ya miaka mitatu akisema wameona mambo mengi aliyoacha Hayati Dk. Magufuli yanaendelezwa kwa kasi kubwa na Rais Samia.

Kevela anataja baadhi ya masuala makubwa ya kitaifa yaliyofanywa na Rais Samia tangu alipoingia madarakani kuwa ni pamoja na kuendeleza miradi ya kimkakati ikiwemo ya ujenzi wa Bwawa la kuzalisha umeme la Mwalimu Nyerere, ujenzi wa Reli ya Kisasa, madaraja makubwa kama la Kigongo – Busisi mkoani Mwanza na mengine.

Anasema mafanikio mengine ni kuimarisha diplomasia ya kiuchumi hatua iliyowezesha kufungua fursa mbalimbali za uwekezaji, mitaji, masoko ya bidhaa, ongezeko la watalii.

"Tukiangalia ujenzi wa miundombinu amejenga vituo vya afya, majengo ya mama na mtoto, madarasa, madaraja, miundombinu ya maji nchi nzima, ameboresha viwanja vya ndege na kuongeza ununuzi wa ndege, miradi ya kimkakati kama vile SGR, Bwawa la Mwalimu Nyerere yote inaendelea vizuri.

"Royal Tour katufanyia vizuri watalii wameongezeka, pato la nchi limeongezeka, utawala bora ameiukuza diplomasia nchi yetu sasa inang'ara kimataifa.

"Nchi imekuwa na utulivu na amani, mfanyabiashara amka fanya biashara yako, ameimarisha michezo kwa kuwapa motisha wachezaji na sasa tunakwenda kuwa mwenyeji wa mashindano ya Afcon nchi yetu itapanda kimataifa na tutaongeza mapato kwahiyo wafanyabiashara tujiandae," anasema Kevela.

Anasema pia Rais Samia ameiwezesha nchi kuwa na mtangamano wa kisiasa unaojumuisha siasa safi za kistaarabu na zinazoheshimu mawazo wa kila mmoja.

Anasema kulikuwa na tofauti za kisiasa zilizosababisha kutokuwa na majadiliano baina ya chama tawala na vya upinzani lakini tangu Rais Samia aingie madarakani mazungumzo yanafanyika.

"Rais Samia amefungua ukurasa mpya wa siasa na demokrasia lakini kubwa ni fursa ya maridhiano ambayo yanaendelea mpaka sasa. Dhamira yake ya kukutana na vyama vya siasa, mtu mmoja mmoja inaleta faraja kwa wengi.

"Kama mama nasema Samia Suluhu Hassan adumu katika uongozi wake, tunamuunga mkono kwa asilimia mia moja, wanasema mnyonge mnyongeni haki yake mpeni…kazi kaifanya Watanzania tunaiona, mataifa ya nje yanaona.

"Akinamama wenzangu nchi nzima tunataka Mungu atupe nini, atupe kidonda, atupe upele, Rais Samia aendelee kuiongoza nchi hii kwa sababu tunaona anachiokifanya," anasema Kevela.

Anasema pia chini ya uongozi wake Tanzania imepiga hatua katika kuongeza usawa wa kijinsia na kusema ni kielelezo cha mafanikio ambayo mwanamke anaweza kuyafikia.

"Rais Samia aliunda wizara mahususi ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu inayoweka kipaumbele eneo la usawa wa kijinsia. Kwenye teuzi mbalimbali akina mama tumependelewa, wako mawaziri, wakurugenzi, wakuu wa wilaya, makatibu tawala na wengine wengi tunaona namna anavyoendelea kuitafuta ile Hamsini kwa Hamsini," anasema.

Mwenyekiti huyo wa UWT Njombe, anasema Rais Samia amekuwa kielelezo cha mafanikio makubwa yanayofikiwa nchini kwa kuliwezesha Taifa kuendelea kuwa na utulivu na amani.

Kevela anagusia pia sera ya upatanishi, ustahimilivu, mageuzi na ujenzi wa nchi maarufu kama 4R kwamba imefanya hali ya siasa nchini kuwa tulivu.

"Nawasihi Watanzania tupige chini magoti tumwambie Mungu asante kwa kumpata kiongozi bora na tuendelee kumwombea ili aendelee kuongoza nchi hii kwa sababu wanasema ukiichoka amani kitakachofuata tuangalie nchi za wenzetu.

"Nchi ambazo zinakosa amani na utulivu ni vita kila wakati, shida wanaozipata ni mwanamke, mtoto na mzee kwa sababu mwanamke hajaumbiwa kukimbia familia. Vita inapotokea mama atafia kwa watoto, wazee watashindwa kukimbia.

"Kwahiyo tuendelee kumuombea nchi iendelee kutulia, mimi nasema mitano tena kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Njombe," anasema Kevela.

Kevela pia anataja baadhi ya mafanikio yaliyopatikana mkoani Njombe tangu Serikali ya Awamu ya Sita ilipoingia madarakani ni pamoja na uboreshwaji wa huduma mbalimbali za kijamii kama vile za afya, elimu, maji, miundombinu ya barabara na kilimo na kuwawezesha wananchi kupata maendeleo.

"Njombe tunalima sana na mafanikio ambayo tunajivunia tangu mama Samia aingie madarakani kwa sekta ya kilimo ni upatikanaji wa mbolea za ruzuku. Tumeona jitihada za serikali katika kutoa ruzuku ya mbolea, mbegu na viuatilifu kwa mazao ya kimkakati kama vile pamba, korosho, alizeti, chikichi, kahawa na chai," anasema Kevela.

**NAMBA ZINAONGEA**

Katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia vipaumbele mbalimbali vimetekelezwa kwa serikali kutoa fedha zilizowezesha kufikiwa kwa malengo ya vipaumbele husika.

Mathalani katika sekta ya afya Sh trilioni 6.722 zimetumika kutekeleza vipaumbele mbalimbali ili kuimarisha huduma za afya nchini kama vile ujenzi wa miundombinu ambao umewezesha kuongezeka kwa vituo vya kutolea huduma za afya kutoka 8,549 mwaka 2021 hadi kufikia 9,610 Machi 2024 sawa na ongezeko la vituo 1,061.

Bajeti ya kilimo imeongezwa kutoka Sh bilioni 751 (2022/2023) hadi Sh bilioni 970 (2023/2024) ambalo ni ongezeko la asilimia 29 ili kuongeza tija na kupunguza gharama za uzalishaji kwa wakulima na kuhakikisha usalama wa chakula.

Hatua hiyo imewezesha kuongezeka kwa wzalishaji wa mazao ya chakula kutoka tani 17,148,290 kwa msimu wa 2021/2022 hadi tani 20,214,000 (2022/2023) ambapo kiwango cha utoshelevu wa chakula ni asilimia 124.

Katika sekta ya utalii takwimu zinaonyesha kwa mwaka 2023 watalii walioingia nchini ni 1,750,557 ikilinganishwa na watalii 1,381,881 wa mwaka 2022 huku mapato yakifikia Dola bilioni 3.22 ikilinganisha na Dola bilioni 2.33.

Vilevile ushawishi wa Tanzania kidiplomasia umeongezeka maradufu katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Samia hatua iliyoongeza kiwango cha uwekezaji ulioingia nchini kutoka Dola bilioni 1.03 mwaka 2020 hadi kufikia Dola bilioni 5.6 mwaka 2023.



# Asia, Afrika soko kubwa la bidhaa za Tanzania

NA MWANDISHI WETU, DAR ES SALAAM



NCHI za Bara la Asia na Afrika zimetajwa kuwa fursa kubwa kwa bidhaa na mazao yanayozalishwa nchini Tanzania kuliko za Ulaya Magharibi.

Hayo yameelezwa jijini Dar es Salaam jana na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade), Bi. Latifa Mohammed Khamis, wakati akizungumza na wahariri wa vyombo vya habari. Bi. Khamis alisema, mataifa ya Asia na Afrika hayana masharti magumu kama yalivyo yale ya Magharibi, ambayo hata kama bidhaa zitatimiza vigezo lakini hutafuta kasoro ndogo tu ili kuwakwamisha wafanyabiashara wa Tanzania na nchi nyingine za Afrika.

Akizungumzia mafanikio ya utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka hiyo kwa mwaka 2022/2023, alisema kwamba TanTrade imeratibu matukio mbalimbali ikiwemo programu za utafiti, makongamano na misafara ya kibiashara, maonesho na mikutano ya kuunganisha wazalishaji na wanunuzi.

Alisema, katika soko la Kenya, jumla ya kampuni 54 zilishiriki ambapo mazao ya kipaumbele yalikuwa bidhaa za vyakula, nafaka, mbao na mashudu, wakati kwenye soko la Uturuki, kampuni 50 zilishiriki huku bidhaa zikiwa Pamba, ngozi, viungo na mbogamboga.

Aidha, jumla ya kampuni 15 zilishiriki nchini Comoro huku mazao ya kipaumbele yakiwa nafaka, mifugo, mbogamboga, vifaa vya ujenzi, vyombo vya nyumbani na matunda, na katika soko la Saudia kampuni 9 zilishiriki kuuza Cocoa, Kahawa, Chai, Korosho, nyama na asali.

Kwa soko la Oman, jumla ya kampuni 300 zilishiriki, ambapo bidhaa zilikuwa nyama, nafaka, mbegu za mafuta, mbogamboga na matunda, wakati kampuni 271 zilishiriki Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo zikiwa na mazao ya kipaumbele kama mahindi, maharage, mtama, mchele, unga wa mahindi, bidhaa za viwandani na huduma za teknolojia.

"Sudan Kusini jumla ya kampuni 55 zilishiriki kuuza mahindi, maharage, mtama, mchele, unga wa mahindi, bidhaa za viwandani, elimu, teknolojia, afya, na viwango vya ubora, wakati nchini Afrika Kusini kampuni 16 zilipata fursa zikiwa na bidhaa za kahawa, korosho, asali, utalii, bidhaa za chuma na vifaa vya umeme," alisema.

Kwa ziara ya Malawi, kampuni 150 zilishiriki huku mazao ya kipaumbele yakiwa kilimo, uvuvi, uchumi wa buluu, uzalishaji utalii, huduma za fedha, uchukuzi, miundombinu, mawasiliano, madini, elimu na afya.

Alisema, kupitia matukio hayo, baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni kampuni ya Akros Cashew ya Tanzania iliuza tani 37 za korosho zenye thamani ya Dola za Kimarekani 202,700 kupitia maonesho yaliyofanyika nchini Afrika Kusini. "Kampuni za Tanzania zilifanikiwa kufanya mauzo ya papo kwa papo yenye thamani ya Dola za Kimarekani 100,000 kwa bidhaa mbalimbali za kilimo na pembejeo kupitia msafara wa Malawi ambapo pia kampuni nyingine ziliweza kupata miadi ya mauzo yenye jumla ya thamani ya Dola za Kimarekani milioni 20.3 kupitia msafara huo wa Malawi," alisema.

***Hadi Agosti, 2023 TanTrade imekamilisha rajamu ya iliki, tangawizi, mdalasini, pilipili manga na karafuu vilevile, Mamlaka inaendelea na taratibu za kukamilisha rajamu za bidhaa nyingine ikiwemo asali, korosho, kahawa na chai,"***

Alizitaja bidhaa zilizotafutiwa masoko katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2018 hadi 2022 kuwa ni, nyama, mchele, soya, karanga, parachichi, pilipili, muhogo, mahindi, karafuu, asali, mbegu za maboga, korosho na zabibu na kwamba nchi zinazoongoza kwa kununua bidhaa hizo ni Qatar, Falme za Kiarabu, Oman, Kenya, Uganda, Rwanda, India, China, Uholanzi, Indonesia, Afrika Kusini, Iran, Ujerumani, Burundi, Singapore, Ireland, Marekani, Vietnam, Ghana, Comoro na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo. Kuhusu mapato ya Mamlaka kwa kipindi cha miaka mitano, Bi. Khamis alisema, TanTrade ilipanga kukusanya jumla ya Shs. 52,562,298,340 na ikafanikiwa kukusanya Shs. 40,004,650,548 sawa na asilimia 76, kutoka vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na ruzuku kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya mishahara na miradi ya maendeleo na vyanzo vya mapato ya ndani ikiwemo ada inayotozwa kwenye uratibu na usimamizi wa Maonesho, upangaji wakati usio wa Maonesho pamoja na ushiriki na viingilio vya Maonesho ya DITF.

Katika kipindi hicho cha miaka mitano, Bi. Khamis alisema, walitoa kiasi cha Shs. 627,548,541.17 kama gawio la mapato kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali, ikiwa ni asilimia 20.15 ya kiasi kilichokusudiwa kupatikana cha Shs. 3,113,830,095.71.

Kwa upande mwingine, Bi. Khamis alisema, taasisi inaendelea kufuatilia utekelezaji wa mikataba na makubaliano ya kibiashara iliyosainiwa katika matukio mbalimbali yaliyoratibiwa na TanTrade.



Aliongeza kuwa, katika kipindi cha miaka mitano ilisainiwa jumla ya mikataba 46 yenye thamani ya Shs. trilioni 17.53. "TanTrade imekamilisha maombi ya ufadhili ya kuendeleza rajamu ya Taifa ya Viungo (Tanzania Spice Label) kwa kushirikiana na Kituo cha Biashara cha Kimataifa (ITC) pamoja na wadau wa sekta ya viungo.

"Hadi Agosti, 2023 TanTrade imekamilisha rajamu ya iliki, tangawizi, mdalasini, pilipili manga na karafuu vilevile, Mamlaka inaendelea na taratibu za kukamilisha rajamu za bidhaa nyingine ikiwemo asali, korosho, kahawa na chai," alisema.

Katika kuendelea na kutafuta masoko ya bidhaa zinazozalishwa nchini, alisema TanTrade imefanya uchambuzi wa takwimu katika mfumo wa ITC kutambua bidhaa zinazohitajika kwenye masoko mbalimbali duniani. Nchi ambazo zinahitaji bidhaa hizo ni pamoja na India, Umoja wa Falme za Kiarabu, Uswisi, Vietnam, China, Pakistani, Japani, Marekani, Oman, Qatar, Kuwait na Saudi Arabia.

Aliitaja mikakati ya utekelezaji kwa mwaka 2023/2024 kuwa ni kuendelea kuratibu shughuli za utafutaji masoko na ukuzaji biashara ili kuunganisha wazalishaji, kuimarisha upatikanaji wa taarifa za kiintelijensia za biashara, na kuimarisha Ofisi ya Zanzibar ili kuendeleza na kutafuta masoko ya bidhaa za kipaumbele.

Mikakati mingine ni, kuendelea na taratibu za uanzishwaji wa Dawati la Waambata wa Kibiashara kwenye Balozi za kimkakati za Tanzania nje ya nchi, kuimarisha na kukuza biashara za mipakani, kuratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Maonesho ya Expo 2025 Osaka, Japan, na kuendeleza ushirikiano na Balozi nje ya nchi katika kutangaza fursa za masoko ya bidhaa na mazao yanayozalishwa nchini.

# Jinsi magenge yalivyoibuka na kuitawala Haiti

NA BBC SWAHILI

MAELFU ya wafungwa wamekuwa huru baada ya magenge kuvamia jela na kuwaachia huru, katika nchi yenye serikali isiyo na afisa hata mmoja aliyechaguliwa na raia na kiongozi wa genge ambaye alikuwa anamtishia waziwazi waziri mkuu Ariel Henry ambaye tayari amekwishaachia ngazi.

Matukio yanayoendelea nchini Haiti yanawashtua hata wale wanaofuatilia kuongezeka kwa makundi yenye silaha nchini humo katika miaka ya hivi karibuni.

Hapa tunaangalia kwa undani jinsi magenge yalivyoibuka na kutawala maeneo makubwa ya mji mkuu na maeneo ya vijijini ya nchi hiyo ya Caribbean.

Makundi yenye silaha kwa muda mrefu yamekuwa yakihusika na umwagaji damu katika historia ya Haiti.

Wakati wa miaka 29 ya udikteta wa François Duvalier, anayejulikana kama Papa Doc, na mwanawe Jean Claude "Baby Doc" Duvalier, kikosi cha kijeshi kilichoitwa Tonton Macouse kilitumia vurugu kali kukomesha upinzani wowote kwa utawala wa Duvalier.

Duvalier mdogo alilazimishwa kwenda uhamishoni mwaka 1986, lakini magenge yamekuwa yakipata nguvu kila uchao na wakati mwingine yakilindwa na kuhamasishwa na wanasiasa wanaoshirikiana nao.

## MAUAJI YA RAIS MOÏSE

Mlipuko wa sasa wa ghasia za magenge umechochewa na mauaji ya Rais Jovenel Moïse tarehe 7 Julai 2021.

Rais huyo aliuawa kwa kupigwa risasi na kundi la mamluki wa Colombia nyumbani kwake nje ya Port-or-Prince.

Wakati raia hao wa Colombia na washukiwa wengine kadhaa wakikamatwa, uchunguzi wa mauaji yake bado haujabaini ni nani aliamuru kuuawa kwa rais huyo. Vurugu za magenge tayari zilikuwa zimekithiri chini ya Rais Moïse, lakini ombwe la mamlaka lililotokana na mauaji yake liliruhusu magenge kuteka maeneo zaidi na kuwa na ushawishi zaidi.

Na sio tu nafasi ya rais ambayo iko wazi: Kufuatia kucheleweshwa mara kwa mara kwa uchaguzi wa wabunge, mihula ya viongozi wote waliochaguliwa yameisha, na kuacha taasisi za nchi zikiwa hazina usukani.

Tangu mauaji ya Jovenel Moïse, nchi hiyo imetawaliwa na Ariel Henry.

Henry alikuwa ameteuliwa na Rais Moïse kama waziri mkuu wake muda mfupi kabla ya kuuawa, lakini hajachaguliwa na raia na kwa hiyo baadhi wanatilia shaka uhalali wake.




Upinzani dhidi ya uongozi wa Ariel Henry ulikuwa ukiongezeka huku chaguzi alizoahidi kufanya zikishindwa kutekelezwa.

Isitoshe, ukosefu wa usalama umeongezeka, na kuwalazimu maelfu ya raia wa Haiti kukimbia makazi yao.

## MAGENGE YA HAITI

Mmoja wa wapinzani wakuu wa Henry ni Jimmy Chérizier, afisa wa zamani wa polisi ambaye amekuwa kiongozi wa genge baada ya kutimuliwa na jeshi la polisi.

Anajulikana kwa lakabu ya Barbecue, askari huyo wa zamani anaongoza genge la G9, muungano wa magenge tisa yaliyoanzishwa mwaka 2020 ambayo yanaripotiwa kuwa na uhusiano na Chama cha marehemu Rais Moïse cha Tèt Kale.

Barbeque alitumia mauaji ya Moïse, ambapo anawalaumu mabwanyenye kwa mauaji hayo na kuwahimiza wafuasi wake kushiriki katika kile alichokiita "vurugu halali."

Mashambulizi ya kikatili na uporaji yameenea, haswa katika mji mkuu, Port-or-Prince, ambapo Barbeque ana ngome zake.

Mwezi Oktoba 2021, Ariel Henry alizuiwa kuweka shada la maua kwenye mnara wa Moise, wakati wanachama waliokuwa wamejihami na silaha wa genge la Barbeque walipojitokeza ghafla na kufyatua risasi hewani.

Akiwa amevalia suti nyeupe na pembeni yake akiwa na watu wake, Barbeque aliweka shada la maua kwenye mnara huo – katika tukio la kuonyesha nguvu zake.

Genge lake la G9 pia limekuwa likipigana vita vya umwagaji damu na G-Pèp, genge pinzani ambalo linahusishwa na vyama vilivyompinga Rais Moïse.

Shule na hospitali zimelazimika kufungwa na zaidi ya watu 100,000 walikimbia makazi yao mwaka 2023, kulingana na Shirika la Kimataifa la Uhamiaji.

Kamati ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu iliiambia BBC wafanyakazi wake walilazimika kuzungumza na mamia ya magenge ili kuweza kutoa misaada ya kibinadamu.

Katika kunyoosha misuli yake, genge la G9 pia lilizuia usafirishaji wa mafuta mwaka 2022, na kusababisha uhaba wa mafuta na pia kutatiza usafirishaji wa dawa na maji ya kunywa.

Jeshi la polisi la taifa la Haiti - ambalo kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2023 lina maafisa 9,000 pekee katika nchi hiyo yenye wakazi milioni 11 - limejitahidi kukabiliana na magenge hayo, ambayo yamejihami kwa silaha zinazoingizwa kinyemela kutoka Marekani. Asilimia 80 ya mji mkuu uko chini ya udhibiti wa magenge na watu wanaoishi katika maeneo haya wanakabiliwa na ukatili mbaya, kulingana na mratibu wa misaada ya kibinadamu wa Umoja wa Mataifa, Ulrika Richardson.

Bi Richardson anasema kumekuwa na ongezeko la 50% la unyanyasaji wa kingono kati ya 2022 na 2023, huku wanawake na wasichana wakilengwa na magenge hayo.

## UINGILIAJI KATI KUTOKA NJE

Henry alikuwa amerudia wito wa kuungwa mkono kimataifa ili kukabiliana na ghasia hizo, lakini hadi sasa ni Bahamas, Bangladesh, Barbados na Chad pekee ambazo zimeuambia rasmi Umoja wa Mataifa kwamba wanapanga kutuma maafisa wa usalama. Lakini hakuna afisa aliyefika hadi sasa.

Wakati wa ongezeko la ghasia za sasa, Henry alikwenda Kenya kushawishi maafisa ili kutimiza ahadi yao ya kupeleka maafisa 1,000 wa polisi nchini Haiti.

Wakati raia wa Haiti wanatamani usalama, kutumwa kwa maafisa wa kigeni wa usalama kunatazamwa kwa wasiwasi na baadhi ya watu.

Haiti, ambayo ilipata uhuru kutoka kwa Ufaransa baada ya mafanikio ya uasi wa watumwa 1791, ilitawaliwa na Marekani kutoka 1915 hadi 1934. Uingiliaji kati wa kijeshi wa Marekani kati ya 1994 na 2004 pia umewafanya wengi kuwa na wasiwasi kuhusu uingiliaji kati kutoka nje.

Baadhi ya wakosoaji wa Henry wanadhani anataka kuwatumia polisi wa Kenya kuimarisha mamlaka yake, huku maandamano ya kumtaka ajiuzulu yanazidi kuongezeka.

Barbeque ni mmoja wa wale ambao wamemshutumu Ariel Henry kwa kujaribu kuimarisha mamlaka yake kwa kuwaalika maafisa wa usalama wa kigeni.

Mwaka 2022, kiongozi huyo wa genge aliweka mpango wake mwenyewe wa "amani," akipendekeza wanachama wa genge lake wapewe msamaha na baraza la wazee liundwe na wawakilishi kutoka mikoa 10 ya Haiti.

Pia alipendekeza genge lake lipewe nyadhifa katika baraza la mawaziri.

Tangu wakati huo, amekuwa akiongeza shinikizo, akijaribu kujidhihirisha kama "mwanamapinduzi" anayelenga kupindua anachosema ni kiongozi "haramu."

Tarehe 1 Machi, Chérizier alisema angeendelea kupigana na Ariel Henry. "Vita vitadumu kadri inavyohitajika," aliongeza. Tayari Henry amekwishatangaza kujiuzulu wakati maelfu ya wafungwa wakitoroka gerezani.



# Asilimia 98 ya nyoka hawana madhara kwa binadamu

NA MWANDISHI WETU



KUKOSEKANA kwa uelewa wa kutosha juu ya tabia na maisha ya viumbe pori kunachangia kwa kiasi kikubwa mgongano baina ya binadamu na Wanyamapori.

Kwa miaka mingi kumekuwa na mtazamo hasi kwa binadamu hasa wanaoishi pembezoni mwa hifadhi na mapori ya akiba nchini kudhani kuwa wanyama ndio chanzo cha migongano kwenye maeneo wanayoishi.

Ukweli ni kwamba kwa kiwango kikubwa binadamu ndio wamekuwa kisababishi cha migogoro hiyo kutokana na kuanzisha makazi kwenye mapito ya wanyama au kwenye malisho yao.

Aidha mwenendo wa idadi kubwa ya binadamu kudhani kuwa kila kiumbe pori ni hatari kwa maishayao unachangia migongano zaidi.

Tafiti zinaonesha kuwa viumbepori wengi si wepesi wa kuwadhuru binadamu mahali ambapo hawajachokozwa ama kusumbuliwa kwa namna yeyote.

Pamoja na mambo mengine wapo viumbe pori ambao pamoja na kuwa na sumu kwenye miili yao, lakini hawana madhara kabisa kwa binadamu.

Nyoka wengi ambao idadi kubwa ya Watanzania inawaona kama adui kwao bila kujali aina yake ni moja ya viumbe pori visivyo na madhara kwa binadamu.

Katika aina 3,000 za nyoka wote duniani ni aina 200 tu za nyoka ndio wenye sumu huku aina 2800 wakiwa hawana sumu kabisa.

Aina hii ya nyoka 200 wenye sumu huitumia kwa lengo la kuwinda, kusaidia mmeng'enyo wa chakula na kujilinda dhidi ya adui na wale wasio na sumu hutumia njia mbadala kuhakikisha wanapata chakula na kujilinda.

Jamii zote za Chatu ni miongoni mwa Nyoka wasio na sumu na hujipatia chakula kwa kulinyonga windo lake na kulivunjavunja kabla ya kulimeza na kadiri windo linavyovuta pumzi ndivyo chatu huongeza bidii ya kunyonga.

Mbali na kutafuta chakula, Nyoka wasio na sumu hujikinga na maadui kwa kuwang'ata ili kusababisha maumivu, kujifananisha na mazingira, kujiviringisha ili kuficha kichwa, kutetemesha mkia na wengine hujisugua magamba ili kutoa sauti ya kumtisha adui na hatari inavyokuwa kubwa nyoka hukimbia kwa usalama wao.

Mtaalamu wa masuala ya migongano baina ya Binadamu na Wanyamapori, John Noronha amewaambia Waandishi wa Habari Februari 22, 2024 kuwa nyoka si adui wa binadamu na ukweli ni kwamba kati ya asilimia 100 ya nyoka ni asilimia 30 tu ndio wenye sumu inayoweza kumuua binadamu.

Noronha ameyasema hayo katika mafunzo ya siku mbili ya waandishi wa habari yaliyoandaliwa na JET kwa ufadhili wa Mradi wa Kupunguza Migogoro Baina ya Binadamu na Wanyamapori Tanzania, unaotekelezwa na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ) kwa niaba ya Serikali ya Ujerumani (BMZ).

Amesema nyoka ni kiumbe mpole sana, ambae hawezi kuanzisha mashambulizi kwa binadamu kama hajachokozwa na kwamba nyoka wengi wanang'ata lakini hawana sumu.

"Kabla sijapata elimu ya masuala ya uhifadhi, nilikuwa nawaona nyoka kama adui, lakini baada ya kupata elimu, sitamani kuua hata sisimizi, kwa sababu wadudu na viumbe pori si adui wa binadamu, tunaweza kuendelea kuishi nao kama ilivyokuwa katika miaka yote. "Hakuna sababu ya kudhuru wanyama kwa namna yeyote ile, si nyoka tu, hata wanyamapori hawaleti madhara mahali bila ya kuchokozwa," alisema Noronha.



Mtaalamu wa masuala ya migongano baina ya Binadamu na Wanyamapori, John Noronha.

## NYOKA HAWANA HASIRA

Mhifadhi Wanyamapori Tarafa ya Mikumi wilayani Kilosa mkoani Morogoro, Makene Ngoroma amesema kuwa watu wengi wanafikiri kuwa nyoka wana hasira na filamu nyingi zimetengenezwa kuakisi hilo.

Ukweli ni kwamba nyoka hana kumbukumbu nzuri, hana uwezo wa kuhifadhi kumbukumbu, hajaumbwa kuuma binadamu, mashambulizi mengi ya nyoka ya kumuuma mtu yanatokea kama akihisi tu hayuko salama, anahisi maisha yake yako hatarini.

"Ni kweli nyoka wengi hawana madhara kwa binadamu, binadamu tunapaswa kujua kuwa nyoka hawawezi kutafuna chakula chao ingawa wanaweza kumeza wanyama wakubwa kuliko vichwa vyao. Muundo wa taya zao unafaa kwa hilo."

## NYOKA WOTE WANANG'ATA

Ofisa Uhifadhi kitengo cha uchunguzi kutoka TAWA, Tryphone Kanon amesema kuwa nyoka wote wanang'ata, lakini si wote wanaong'ata wana sumu.

Kanon alisema hata wale wenye sumu ziko nyakati wanang'ata bila kutoa sumu badala yake hujeruhi kwa nia ya kujilinda baada ya kuona uwepo wa hatari kubwa mbele yake.

## TAHADHARI

Mtaalamu wa afya, Dkt. Damas Mavika amesema kuwa pamoja na ukweli huo kuwa nyoka wengi hawana madhara kwa binadamu, ipo haja ya kuchukua tahadhari hasa ya kutochokoza nyoka na viumbe pori wengine.

Dkt. Mavika pia alitoa maelekezo kwa mtu atakayeng'atwa na nyoka kuhakikisha anatafuta matibabu kwa haraka.

"Usijajiribu kukamata nyoka kama huna utaalamu huo kwa sababu nyoka wengi hawapendi kubugudhiwa."

Aidha, wataalamu wa wanyamapori na viumbe pori wanashauri binadamu kutoaua nyoka na viumbe pori bila sababu za msingi, lakini pia waepuke kuvamia maeneo ya wanyama pori hasa malisho na mapito yao.

# China, Marekani zinavyozozana kuhusu madini Amerika Kusini

NA MASHIRIKA YA HABARI

ZAIDI ya nusu ya madini ya lithiam duniani inapatikana Argentina, Bolivia na Chile, pembetatu ya masoko ambayo yamevutia wawekezaji na serikali za kitaifa.

Nchi kama China na Markani zinatafuta kupata vifaa vya chuma muhimu kwa utengenezaji wa betri zinazotumiwa na magari ya umeme, soko linalokua ambalo limevutia wawekezaji wengi zaidi.

"Mamlaka kuu zinapigania kupata madini muhimu kwa mpito wa nishati na Amerika ya Kusini ni uwanja mkuu wa vita," Benjamin Gedan, mkurugenzi wa Mpango wa Amerika Kusini wa Kituo cha Wilson, aliiambia BBC.

"Marekani ilichelewa kwenye karamu na Washington ina wasiwasi kwamba China imetangulia mpango huo," anaongeza.

Makampuni ya China yametumia miaka mingi kutafuta mahali pa kuhifadhi madini hayo yanayoitwa dhahabu nyeupe katika sehemu mbalimbali za dunia, hasa katika Amerika ya Kusini, ambako kuna akiba kubwa zaidi ya madini hayo.

Bolivia inaongoza katika orodha hiyo ikiwa na hifadhi inayokadiriwa kuwa tani milioni 21, ikifuatiwa na Argentina (milioni 19.3) na Chile (milioni 9.6), kulingana na Utafiti wa Jiolojia wa Marekani.

Na Mexico, ingawa ina tani milioni 1.7 tu (iliyo nafasi ya tisa kwenye orodha), imekuwa kiungo muhimu katika eneo la Amerika ya Kaskazini, si tu kwa sababu ya ukaribu wake wa kijiografia na Marekani na Canada, lakini pia kwa sababu inakuwa kituo cha uzalishaji wa magari yanayotumia umeme (hasa baada ya tangazo la hivi majuzi kwamba





kampuni kubwa za magari kama vile Tesla na BMW zitaanzisha viwanda huko).

### MPANGO WA CHILE

Chile ni nchi ya pili duniani kwa uzalishaji wa madini ya lithiam baada ya Australia.

Kufikia sasa, unyonyaji wa rasilimali hiyo umekuwa mikononi mwa kampuni za kibinafsi, lakini mpango mpya uliowasilishwa na Rais Gabriel Boric unatazamia kubadilisha mtindo huu wa biashara na kujiwekea faida ya hiyo Dhahabu Nyeupe nchini.

Pesa nyingi zinazotokana na madini kama vile lithiam hazitokani na uchimbaji wa rasilimali ghafi, lakini kutokana na kuongeza thamani baadaye katika mnyororo wa usambazaji bidhaa - kwa kutumia lithiam kutengeneza betri za umeme, kwa mfano.

Rais wa Chile anatazamia kuanzisha ushirikiano wa sekta ya umma na binafsi ambapo serikali inashikilia hisa inayodhibiti, na kukuza maendeleo ya teknolojia ili kuiweka Chile ndani ya msururu wa ugavi wa sekta inayositawi.

Lakini hii haitakuwa changamoto rahisi, kwani sehemu kubwa ya dunia inajaribu kunyakua kipande kikubwa cha mkate huo.

### 'SHUGHULI MBAYA'

Jenerali Laura Richardson, kamanda wa Kamandi ya Kusini mwa Marekani, alionya kwamba China "inaendelea kupanua ushawishi wake wa kiuchumi, kidiplomasia, kiteknolojia, habari na kijeshi katika Amerika ya Kusini na Caribbean," wakati alipofika mbele ya Kamati ya Huduma za Silaha ya Baraza mnamo Machi kuwasilisha ripoti yake.

"Eneo hili limejaa rasilimali nyingi na nina wasiwasi na vitendo viovu vya wapinzani wetu wanaojinufaisha kwa kujifanya wanawekeza kumbe wanafanya shughuli ya uchimbaji," alisema.

Akizungumzia juu ya "pembetatu ya lithiam" ya Amerika Kusini - inayojumuisha Argentina, Bolivia na Chile, alisema kuwa "uchokozi wa China na njama ya kunyakua lithiam ni ya hali ya juu na ni kali sana".

### CHINA INASEMA NINI?

Waziri wa Maliasili Wang Guanghua amesema, "China ina utegemezi mkubwa wa kigeni kwa baadhi ya rasilimali muhimu za madini, na mara hali ya kimataifa itakapobadilika, hakika itaathiri usalama wa kiuchumi au hata usalama wa taifa," Waziri wa Maliasili Wang Guanghua alisema mapema Januari katika mahojiano na shirika la habari la kitaifa, Xinhua. Serikali imejumuisha madini 24 ya kimkakati katika Mpango wake wa Kitaifa wa Rasilimali ya Madini, uliochapishwa mwaka 2016.

Baadhi ya madini hayo ni pamoja na chuma, shaba, aluminium, dhahabu, nikeli, cobalt, lithiam, na ardhi adimu, pamoja na rasilimali za jadi za nishati kama vile mafuta, gesi asilia, gesi ya shale na makaa ya mawe.

Mpango huo unabainisha kuwa madini ni muhimu katika "kulinda usalama wa uchumi wa taifa, usalama wa ulinzi wa taifa, na maendeleo ya viwanda vinavyoibukia kimkakati".

### ONGEZEKO KUBWA LA UWEKEZAJI WA CHINA

Wakati makampuni ya China yanaendelea katika Amerika Kusini na uwekezaji mkubwa wa madini, nchi tatu zilizo na idadi kubwa ya madini ya hayo zinakusudia kuchukua fursa ya teknolojia na mtaji wa makampuni ya Kichina ili kukuza maendeleo ya viwanda vya ndani.

Katika miezi mitatu ya kwanza ya mwaka huu pekee, makampuni ya China yametia saini mikataba kabambe ya kuwekeza katika nchi za Bolivia, Argentina na Chile.

Katika miezi mitatu iliyopita, China imetangaza uwekezaji mkubwa katika Amerika ya Kusini. Nchini Bolivia, makampuni ya Kichina ya CATL, BRUNP na CMOC yamejitolea karibu dola bilioni mja ($1bn) katika miradi ya lithiam katika idara za Potosí na Oruro, kulingana na Taasisi ya washauri wa Atalantiki wa masuala ya kibiashara na kiuchumi.

Nchini Argentina, kampuni ya Chery Automobile itawekeza kiasi cha dola milioni 400 katika ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza magari ya umeme, ikiwezekana huko Rosario.

Na nchini Chile, Tsingshan Holding Group, Ruipu Energy, Battero Tech, na FoxESS wamejitolea kuwekeza katika bustani ya viwanda vya lithiam katika jiji la Antofagasta, kwa kiasi ambacho bado hakijajulikana.

Uhusiano wa kibiashara kati ya Argentina na Uchina umezidi kuwa wa karibu katika uchimbaji madini ya lithiam, na tangazo la angalau miradi tisa ya uwekezaji mnamo 2022 pekee katika maeneo ya Salta, Catamarca, na Jujuy.

### USHINDANI WA KITEKNOLOJIA NA KIJIOGRAFIA KATI YA MATAIFA MAKUBWA

Kulingana na mkurugenzi msaidizi wa Kituo cha Amerika ya Kusini cha Adrienne Arsht cha Taasisi ya Sera ya Atlantiki, Pepe Zhang, "Marekani inatafuta kikamilifu kuimarisha nafasi yake katika usambazaji wa kimataifa na ugavi wa madini muhimu na teknolojia ya kijani."

Hii ina maana kwamba "lithiam inathibitisha kuwa eneo muhimu zaidi katika ushindani wa kiteknolojia na kijiografia kati ya Marekani na China," aliiambia BBC. Na China inapiga hatua kwa kasi katika.



# Licha ya uzuri wake maeneo haya matano duniani mwiko kuyatembelea

NA BBC SWAHILI

DUNIA imebarikiwa kuwa na maeneo mengi ya kuvutia, ambayo hukusanya watu wa mataifa mbalimbali kuyatembelea. Kawaida vivutio vigi vinawekewa utaratibu ukiwemo wa utuzaji na malipo. Mwaka 2019, sekta ya utalii duniani ilichangia asilimia 10.4% ya pato ghafi la dunia. Lakini yapo maeneo mazuri yangeweza kuchanfgia zaidi, ila ni marufuku kukanyaga.

Mamilioni ya watalii hutembelea hifadhi za wanyamapori, milima mirefu, majumba ya kale, maeneo ya utamaduni na maeneo mengine yanayowavutia. Lakini yapo maeneo duniani ambayo watalii wangetamani kutebelea lakini kwa sababu ya sifa zake na historia yake yanaleta kikwazo. Mengi yamekuwepo bila kutunza kitalii lakini yanavutia kwa historia yake na vilivyomo.

Mengine ni wanasayansi tu huruhusiwa kuyafikia kwa masharti maalumu, maeneo mengine wala hukatazwi kuyatembelea lakini yanahitaji moyo wa kipekee kuyatembelea.

Kwa wenye imani, wengine wanasema kuwepo kwa maeneo ya aina hiyo kunaonyesha ukuu wa uumbaji wa Mungu. Ingawa yapo maeneo zaidi ya 30 yenye sifa hizi, lakini BBC inakuletea orodha ya maeneo sita ambayo watalii mwiko kuyatembelea licha ya uzuri na historia ya kuvutia ya maeneo hayo.

**1. MAPANGO YA LASCAUX, UFARANSA**

Haya ni mapango marefu yanayopatikana Kaskazini mashariki mwa Ufaransa. Ni moja ya mapango ambayo kunapatikana michoro mizuri na maarufu zaidi kwenye kihistoria duniani. Inaelezwa ni michoro ya siku nyingi ya enzi za mababu wa mababu ikitajwa kuwa ina miaka zaidi ya 17,000. Michoro mingi ni ya wanayama wakubwa wakubwa ambao wanatajwa waliishi miaka hiyo katika maeneo hayo. Mapango hayo yameorodheshwa na kutambulika naShirika la Umoja wa Mataifa la elimu, sayasi na Utamaduni (UNESCO) kama urithi wa dunia.

Nyumba ni bure na ni nzuri ,lakini hakuna anayetaka kuishi katika paradiso hii,kunani?

Hata hivyo toka mwaka 2008 mapango hayo yamefungwa kutokana na mlipuko wa fangasi wanaotoko kwenye mapango hayo. Wakiruhusiwa wasayansi wachache sana angalau mara oja moja kwa mwezi kwa lengo la kutafiti.

**2. KISIWA CHA NORTH SENTINEL, INDIA**



Ni kisiwa kidogo sana chenye msitu mnene zaidi kwenye ghuba ya Bengal. Ni moja ya visiwa vya Andaman kwenye bahari ya Hindi, kilichozungumza na miamba mikubwa ya mawe ya matumbawe, hali inayoleta ugumu kukifikia kwa njia ya boti.

Lakini hicho sio kikwazo pekee cha watu kutoruhusiwa kufika ama kushindwa kutembelea, kikwazo kikubwa ni kwamba kisiwa hicho ni makazi ya watu wa jamii ya Sentinel ambao hawataki muingiliano na watu wengine duniani. Inaelezwa ndio jamii iliyosalia duniani ambayo haijaguzwa na maisha ya kileo na dunia ya sasa.

Mwaka 2008, wavuvi wawili ambao boti yao kwa bahati mbaya ilikikaribia kisiwa hicho waliuawa na watu hao. Na mwaka 2004 wakati wa dhoruba kubwa la Sunami, wanasayansi walitumia helkopta kuangalia athari zilizowakumba watu hao. Wakiwa kwenye anga za fukwe walianza kushambuliwa kwa mishale, mikuki na mawe.

**3. DOOMSDAY VAULT, NORWAY**

The Doomsday Vault ni benki ama ghala kubwa la mbegu duniani, linalopatikana nchini Norway. Kila mbegu unayoijua duniani na kutumika kwenye kupata zao inahifadhiwa hapo. Ghala hili liko mbali na makazi ya watu na mahala ambapo hata vita ikitokea ama gharika lolote likitokea mbegu hizo zitaendelea kuwa salama. Sehemu kubwa ya ya ghala hilo iko ardhini na haifikiki kirahisi labda kwa watumishi wachache wanaofanya kazi hapo. Ni eneo lenye baridi sana na kulindwa wakati wote.

4. Poveglia, Italia

Kisiwa kingine kidogo kinachopatikana kati ya Venice na Lido kaskazini mwa Italia. Katika historia ya kisiwa hicho, ni mahala panapopatikana sana ngome kongwe , mahala ambapo palitumika kama kituo cha kuangalia usalama wa meli na baadae pakatumika kama karantini ya kuwahifadhi wagonjwa wenye magonjwa mbalimbali hasa ya mlipuko na magojwa ya akili.

Lakini mwaka 1968, Hospitali iliyokuwa inatumika kwa wagonjwa hao ambao wengi walikuwa wenye magojwa ya akili, ilifungwa na tangu wakati huo, kisiwa hicho kimetelekezwa.

Kuna hisia kwamba tangu kufungwa kwa Hospital hiyo, mizimu ya wagonjwa waliofariki, watu waliouawa kweye vita inaendelea kuwepo kwenye majengo ya kisiwa hicho. Kumekuwana sauti zikisikika kwenye miamba na mawe yaliyoporomoka. Sauti zisizoeleweka. Watu wengi walikacha kwenda kwa hofu. Mwaka 2014 Serikali ya Italia iliwahi kutangaza kukipangisha kisiwa hicho kwa miaka 99 ii kuvutia watu watakaokiendeleza, lakini hofu imetawalazaidi ya kufika huko.



**5: KISIWA CHA NYOKA, BRAZIL**

Kama jina lake lilivyo, Kisiwa cha nyoka chini Brazil (Ilha da Queimada Grande) ni eneo lenye nyoka wengi ma wakali pengine kuliko maeneo yote duniani yenye ukubwa huo. Ni eneo lenye ukubwa wa hekari 43 na nyoka wanaopatikana wanatajwa kuwa na sumu kali zaidina inayoweza kuua binadamu kwa haraka.

Kila mita za mraba tano kuna nyoka, ni sawa na hatua kama tano ukitembea kwa miguu lazima ukutane na nyoka wa ukubwa tofauti. Utafiti unaonyesha kuna nyota zaidi ya 4,000 aina ya Golden Lancehead Viper wanaopatikana kwenye kisiwa hicho kilichoko maili takribani 20 kutoka pwani ya mji wa Sao Paulo. Serikali ya nchi hiyo imepiga marufu binadamu yeyote kutembelea kisiwa hicho kwa sababu ya usalama.

Wanasayansi wachache tena kwa tahadhari kubwa na nyenzo za kisasa za kujilinda wamekuwa wakiruhusiwa kufanya utafiti kila baada ya miaka mitano tena kwa vibali maalumu vya kufa na ama kupona.

# Wakulima wa tumbaku kulipwa ndani ya masaa 48

NA BENNY KINGSON, TABORA



SERIKALI imeyaagiza makampuni ya ununuzi wa zao la tumbaku nchini kuhakikisha inawalipa wakulima pesa zao ndani ya masaa 48 mara baada ya kuchukua mazao yao vinginevyo zitafutiwa leseni ambapo pia imewahakikishia kuwaongezea kuwajengea mabani mapya ili kufanikisha malengo ya kuzalisha tani 200,000 ifikapo mwaka 2025.

Waziri wa kilimo Hussein Bashe akiongea kwa njia ya simu wakati wa ufunguzi wa masoko ya tumbuku kwa kampuni ya ununuzi Mkwawa iliyopo Miemba Manispaa ya Tabora ameyataka makampuni hayo kuwalipa wakulima ndani ya muda huo.

Bashe ameeleza kuwa hakuna sababu ya wakulima kucheweleshewa malipo yao kama ilivyokuwa misimu ya nyuma na kwamba mabenki yote yahakikishe wanakata madeni halisi ya wakulima pasipo kuwakata madeni ya makampuni.

“Makampuni yawalipe wakulima ndani ya masaa 48,mabenki yote yahakikishe ayawakati wakulima madeni ya makampuni,wakate madeni halisi ya wakulima na madeni ya ruzuku wanayodaiwa serikali itayashughulikia mwakani na kuweka mambo sawa”naeleza.

Anaeleza kuwa serikali itahakikisha inawasaidia wakulima kuongeza kujenga mabani mengine ya kuchomea tumbaku ili kuendana na kasi ya uzalishaji na kufikia malengo ya kuzalisha tani 200,000 za zao hilo ifikapo mwaka 2025.

Waziri huyo anayataka makampuni hayo ya ununuzi wa zao hilo kuwafuata wakulima jirani na maghala waliyyohifadhia tumbaku kununua ili kuwapunguzia usumbufu na kwamba wakulima wahakikishe hawachanganyi mazo yao na uchafu katika kulinda ubora na kuleta ushindani wakati wa mauzo.

“Tutapitia upya mfumo wa wateuzi wa madaraja ya tumbaku ili kuondoa kero zilizopo na tutafutilia suala la makampuni kuwalipisha wakulima fedha za miti wakati haipandwi , miti ni lazima ipandwe kwa kuwa zao lenyewe linatumia miti katika kukaushia”anahimiza.

Aliyekuwa Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya tumbaku Hassani Wakasuvi alieleza kuwa zao hilo lina rangi tatu amazzo ni chungwa,limao na kahawia na ilina madaraja matano hapa nchini lakini ya nchini Brazili in madaraja 180 na Zimbabwe 208 na hivyo kuifanya tumbaku ya nchini kuwa bora zaidi.

Wakasuvi ambaye pia alikuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi(CCM )Mkoa wa Tabora na Mjumbe wa halmashauri kuu taifa (MNEC) kutoka Mkoani humo aliwahasa wateuzi wamadaraja kuwatendea haki wakulima kwa kuwa wanahitaji pesa siyo maneno ama uonevu.

Mmiliki wa kampuni ya wazawa ya ununuzi wa zao hilo Mkwawa,Ahamed Mansuli anawataka wakulima kutokuwa na hofu yoyote na watakubali kuwa kampuni hiyo ni bora na yenye uwezo mkubwa kwa kuwa mwaka huu 2023 watanunua tani 145.

Mansuli amnafafanua kuwa kampuni yake imefanikiwa kuwasha mitambo ya kiwanda kilichopo Mkoani Morogoro mapema mwaka jana 2022 na wana uhakika wa kufanya kazi kuwa kwa muda mfupi na kwa ufanisi mkubwa na kwamba watauthibitishi umma kuwa wao ni wazawa halisi.

“Tumejipanga kufanya kazi ya kumkomboa mkulima wa tumbaku na kwa muda mfupi tayari tumeonyesha kuwa uwezo tunao na tutasaidiana na serikali na wakulima wenyewe kuhakikisha malengo ya kuzalisha tani 200,000 ifikapo mwaka 2025 yafanikiwa”anasisitiza.

Mteuzi Mkuu wa Bodi ya tumbaku nchini Albert Charles akisoma taarifa ya maendeleo ya kilimo cha tumbaku Mkoa wa Tabora naeleza kuwa kwa msimu wa mwaka 2021/2022 jumla ya vyama 217 vilishiriki kilimo cha zao hilo ambapo wakulima 18,791 walishiriki.

Charles anafafanua kuwa hadi kufikia mwisho wa masoko tumbaku yote iliyonunuliwa mwaka 2021/2022 ni jumla ya kilo 29,829,742 zenye thamani ya dola za kimarekani 54,025,186.66 na kwamba madeni ya pembejeo kutoka taasisi za kifedha jumla ni dola 26,961,458.92 na baada ya mauzo wakulima walifanikiwa kurejesha jumla ya dola 25,905,723.91.

Anabainisha kuwa malipo ya wakulima baada ya kulipa madeni ya pembejeo yalikua jumla ya dola 28,119,621.44 sawa na takribani shilingi 65,237,521.000 na kwamba wanadai malipo ya msimu 2020/2021 jumla ya dola 1,633,819 ikiwa ni kutoka makampuni ya kizalendo.

Anataja changamoto kuwa ni kutofikiwa malengo ya uzalishaji ambapo malengo kimkoa yalikuwa kilo 31,611,082 za tumbaku lakini hadi kufikia mwisho wa nasoko jumla ya kilo 29,829,742 zimenunuliwa sawa na asilimia 94.4,baadhi ya wakulima kuendelea kuchanganya tumbaku navyama kulaza madeni ya mkopo wa pembejeo. “Changamoto nyingine ni kushindwa kulipa deni la mkopo wa pembejea na pia baadhi ya vyama vya msingi kushindwa kuwalipa wakulima ambapo kumetokana na vyama hivyo kutofikia malengo ya uzalishaji ya mkataba wakati vilitumia mkopo wa pembejeo kwa asilimia 100”anaeleza.

Mteuzi mkuu wa madaraja huyo anataja mafanikio kuwa ni masoko kumalizika mapema mwezi Agosti 2022,kuongezeka kwa makampuni makubwa yaliyoongeza ushindani baina ya makampuni kwenye masoko ya tumbaku na masoko ya pamoja chini ya usimamizi wa Bodi na makampuni yameleta ufanisi mkubwa katika masoko.

Afafanua maendeleo ya kilio msimu wa mwaka 2022/2023 kuwa Mkoa una jumla ya vyama vya msingi 329 vilinavyoshiriki kilimo cha tumbaku,jumla ya wakulima 33,688 walishiriki kilimo cha tumbaku kati ya wakulima 43,278 waliosajiliwa.

Anaendelea kufafanua kuwa makisio ya mkataba wa uzalishaji ni jumla ya kilo 61,732,948 za tumbaku ambazo zilikisiwa kuzalishwa kwenye jumla ya hekta 44,094,makampuni matano yalifunga mkataba na kununua tumbaku kwenye vyama vya msingi .

Anayataja makampuni hayo kuwa ni Alliance One Tobacco Tanzania Limited (AOTTL),Japan Tobacco International Leaf Services (JTILS),Magefa Growers Limited (MGL),Mkwawa Leaf Tobacco Limited (MTL),Voedsel Tobacco Limited (VTL) na chama kikuu cha ushirika WETCU na chama kikuu cha Milambo.

Anaeleza matarajio ya uzalishaji kuwa zoezi la ukaguzi na tathimini ya wingi na ubora wa zao la tumbaku mashambani lilifanyika kuanzia Februari 13 mwaka 2023 hadi Machi 3 mwaka 2023 na kwamba kufuatia ukaguzi huo ilibanika kuwa eneo la hekta 44,586 lilipandwa tumbaku na linaloratajiwa kuzalisha ni kilo 62,287,655.

Anaendelea kueleza kuwa matarajiao ya uzalishaji yaonyesha kuwa kutakuwa na ziada ya kilo 554,707 ikilinganishwa na mkataba na hivyo ni hatua kubwa sana kufikia malengo ya serikali kuzalisha tani 200,000 ifikapo mwaka 2025.

Abainisha kuwa idadi ya AMCOS zilizosajiliwa ni 328,zilizoshiriki ni 329,wakulima waliosajiriwa ni 43,278,walioshiriki ni 33,688. eneo lengwa ni 44,094 na lililopandwa ni 44,586,makisio ni 61,732,948 na matarajio ni 62,287,655 wakati tija ni 1,336 na ziada ni 554,707.

Mkuu wa Mkoa wa Tabora Balozi Dkt.Batrida Burian katika hotuba yake ya ufunguzi wa masoko hayo ya kampuni ya ununuzi ya Mkwawa anaeleza kuwa tumbaku ni zao linaliuheshimisha Mkoa kiuchumi,kibiashara na kimaendeleo kwa wakulima,-jamii na umma kwa ujmla.

Balozi Dkt.Burian anafafanua kuwa mwaka jana 2022 zilizalishwa tani m.29 na mwaka huu tani m.60 ambapo mwaka jana 2022 zilipatikana shilingi B.127 sawa na dola m.56 hivyo ni zao ambalo linaungizia Mkoa mapato makubwa kupitia zao hilo.

Anawasa wakulima kutumia vizuri pesa watakazolipwa kwa kutoa sadaka,-misaada kwa watu wenye uhitaji na watambue wametumia nguvu,muda na fedha zao hivyo wawe waangalifu katika matumizi na kuhakikisha wanaweka akiba kwa ajili ya msimu ujao wa kilimo.

Anahitimisha kwa kuwataka wakulima kutowatumia watoto wadogo kwenye kilimo na endapo watabainika watachukuliwa hatua kali kisheria ikiwa ni pamoja na kupigwa faini na kwa kampuni itayobainika imeshiriki kuwatumikisha watoto kwenye kilimo zitafutiwa leseni.

# Michezo Kimataifa



# Ukweli kuhusu umri wa Wachezaji wa Afrika

LONDON, UINGEREZA

KUMEKUWA na nadharia tofauti kuhusu sababu za wachezaji kujifanya kuwa wadogo kuliko umri wao.

Mwandishi wa habari wa kandanda barani Afrika Oluwashina Okeleji anataja matamanio ya binafsi, shinikizo la kufaulu na urahisi wa kudanganya umri wako kama sababu za kufanya hivyo.

''Ni ngumu sana kwa wachezaji chipukizi kwenda kucheza nje ya nchi na inaweza kuchukua muda mrefu kiasi kwamba wana umri mkubwa sana wanapoonekana, hivyo lazima wapunguze umri labda kwa miaka 10," alisema.

"Sababu nyingine ni shinikizo kwa vijana chini ya umri wa miaka 17 na 20 ili kupata mafanikio. Baadhi ya makocha hawa wanalazimika kusajili wachezaji wenye umri mkubwa zaidi." Mkurugenzi wa zamani wa vyombo vya habari katika Shirikisho la Soka Afrika (Caf) Junior Binyam, anakiri kuwa udanganyifu wa umri ni tatizo barani Afrika kwa sababu nchi hazina kanzidata ya kutegemewa kufuatilia umri.

Alisema: "Ni rahisi katika nchi nyingi kubadili umri au 'kurekebisha' rejista hizo. Si nadra kukuta watu wenye cheti cha kuzaliwa zaidi ya kimoja.

"Katika baadhi ya matukio, mchezaji anapobadilisha utambulisho, anaweza kusajiliwa kama mchezaji mpya.

Udanganyifu wa umri huathiri programu za maendeleo ikiwa wachezaji wanaohusika katika kitengo cha umri sio wa kikundi hicho. "Kutokana na uhaba wa nyaraka za kisheria za kufafanua umri katika Afrika, Koufie anaamini mkanganyiko huo unaweza moja ya sababu ya kile kinachoitwa udanganyifu wa umri.

Alipoulizwa kuhusu ushindi wa Ghana wa Kombe la Dunia la Vijana chini ya miaka 17 mwaka 1991, alikiri baadhi ya wachezaji hawakujua umri wao halisi. Alisema: "watu wengi hawajui walizaliwa lini. Wakati mwingine wanakisia. Ni kweli tuna matatizo Afrika, ndiyo maana tuna shaka kuhusu hilo, iwe ni udanganyifu wa kweli au la."

**TATIZO HILI NI KUBWA KAIASI GANI -** Sio siri kuwa baadhi ya timu za vijana za Kiafrika mara nyingi hushukiwa kuwa na wachezaji waliozidi umri, huku kashfa za umri zikikumba Nigeria, Ghana na Kenya siku za nyuma.

Mchezaji wa zamani wa kimataifa wa Nigeria Jonathan Akpoborie, 54, anasema udanganyifu wa umri "umekithiri" katika soka la Afrika na anaelezea kama "tatizo kubwa" ambalo linakabili mchezo huo.

Mnamo Aprili 2013, wachezaji tisa waliondolewa kwenye michuano ya Afrika ya Vijana wenye umri wa chini ya miaka 17 nchini Morocco baada ya vipimo vya kifundo cha mkono vya MRI kuonyesha kuwa wamevuka kikomo cha umri.

Congo-Brazzaville, Ivory Coast na Nigeria kila moja ilikuwa na wachezaji watatu waliopigwa marufuku.

Baadaye mwaka huo, Nigeria ilipoteza wachezaji kadhaa muhimu kushiriki Kombe la Dunia la wachezaji wa chini ya miaka 17 mwezi Oktoba kwa sababu hiyo hiyo, huku Somalia ikitimuliwa kwenye michuano ya Afrika ya U-17 ya 2013 kwa kuchezesha wachezaji waliozidi umri.

Akpoborie, ambaye sasa anafanya kazi kama wakala, anakiri kuwafahamu wachezaji wengi ambao "walidanganya" kuhusu umri wao katika soka la Afrika.

Aliambia BBC Sport: "Limekuwa tatizo kubwa na bado lipo. Baadhi yao walicheza katika kiwango cha Under-17 na kisha miaka michache baadaye kustaafu kwa sababu hawawezi kukimbia tena.

"Ukiangalia wachezaji wa Kiafrika wanaocheza chini ya umri wa miaka 17, labda mwaka mmoja au miwili baadaye wamestaafu kwa sababu hawawezi kuwasilisha stakabadhi walizotoa katika kiwango cha chini ya miaka 17 kwa sababu umri wao ni mkubwa, wachezaji wasio sahihi wanapewa. jukwaa." Si kwamba hili ni tatizo jipya.

Fifa iliifungia Nigeria kushiriki katika mechi zote za kimataifa kwa miaka miwili baada ya kubaini kuwa tarehe za kuzaliwa kwa wachezaji wake watatu katika Michezo ya Olimpiki ya 1988 zilikuwa tofauti na zile zilizotumiwa na wachezaji hao katika mashindano yaliyopita.

Mnamo 2003, timu ya taifa ya Kenya ya vijana chini ya umri wa miaka 17 ilivunjwa na serikali baada ya baadhi ya wachezaji kukiri kuwa na umri mkubwa.

Je, ni nini kinafanyika kukabiliana na suala hili?

Mnamo mwaka 2009 Shirikisho la Soka Duniani Fifa, lilianzisha matumizi ya picha ya sumaku (MRI) wakati wa michuano ya Kombe la Dunia la Vijana wasiozidi umri wa miaka 17 nchini Nigeria ili kusaidia kujua iwapo wachezaji wamezidi umri au la.

Dk. Yacine Zerguini, Naibu wa Rais wa sasa wa kamati ya matibabu ya Fifa na Caf, alisema wakati huo: "Tunajua kwamba wachezaji hawafanyi hivyo kwa kudhamiria wana zaidi ya miaka 17.


"Katika baadhi ya nchi, vyeti vya kuzaliwa si sahihi au hata havipatikani, bila hiyo kuwa kosa la mchezaji au chama."

MRI hutumika kuchanganua kifundo cha mkono cha kushoto cha wachezaji ili kupata kwa usahihi umri wao halisi.

Binyam alisema kamati ya utendaji ya Caf iliiagiza kamati yake ya matibabu wakati huo kuchunguza kuendeleza matumizi yake kwenye mashindano ya vijana wa chini ya miaka 20.


Wataalamu wa Soka wanasema kuanzishwa kwa uchunguzi wa MRI kumekuwa na mafanikio na pia kusifu juhudi zinazofanywa na serikali binafsi.

Nchini Nigeria serikali kwa mfano imeweka mpango mpya ambapo kila mtoto anayesoma shule anapewa namba maalum ya utambulishoamboa unasalia shuleni.



# Michezo Kimataifa


## Tetesi za soka



LIVERPOOL wameungana na Arsenal na Manchester United kuonyesha nia ya kumnunua winga wa Borussia Dortmund na Uholanzi Donyell Malen, 25. (Bild - in German).



CHELSEA wako tayari kuzingatia kipengele cha kutolewa cha pauni milioni 111 (euro milioni 130) ili kumsajili mshambuliaji wa Napoli mwenye umri wa miaka 25, Victor Osimhen. (Rudy Galetti)




1

HADI kufikia jana jumaapili tunaarifiwa na mtandao wa BBC SWAHILI kuwa Mshambuliajii wa Manchester United Muingereza Marcus Rashford, 26, yuko kwenye orodha fupi ya Paris St-Germain kuchukua nafasi ya Kylian Mbappe, 25, ambaye ana nia ya kuondoka katika klabu hiyo mwishoni mwa msimu.

GALATASARAY wanafikiria kumnunua mlinda mlango wa Manchester United mwenye umri wa miaka 25 kutoka Uturuki Altay Bayindir, ambaye amecheza mechi moja tu tangu ajiunge nayo akitokea Fenerbahce msimu uliopita wa joto. (Sport kupitia Teamtalk)





## Mr Blue msanii bora wa muda wote?

NA MWANDISHI WETU

UKIMTAJA Mr Blue kwenye kizazi hiki cha sasa wengi wao wanaweza kumfananisha au wakahisi msanii ambaye alifanya muziki ilimradi tu kwa sababu anajua kuimba. Kwa watu wanaojua muziki na wameufuatilia muziki tangu zamani ukitaja jina la @mrbluebyser1988 lazima nywele zisisimke kutokana na yale aliyoyafanya kwenye muziki huu wa Bongo Fleva.

@mrbluebyser1988 ni miongoni mwa wasanii bora wa muda wote kutoka hapa Tanzania kutokana na aina ya muziki alioufanya na namna alivyokubalika kwenye jamii. Mr Blue aliwahi kulikamata soko la muziki wa Bongo Fleva na kufanya kila mtu aweze kumzingatia na kuupenda muziki wake pia aliitwa kipenzi cha warembo.

Huyu ndio aliyeaminisha wasanii na jamii kwenye upande wa kuvaa kuwa anajua kuvaa na ndio aliyekuwa na Swaggz kwa uvaaji wake, Uongeaji wake na hata Uimbaji wake. Ni miongoni mwa wasanii waliowahi kukubalika zaidi ndani na nje ya Tanzania lakini kubwa zaidi ni miongoni mwa wasanii walianza muziki wakiwa na umri mdogo zaidi. @mrbluebyser1988 ana zaidi ya miaka 20 kwenye game lakini mpaka leo ana dunda na anaheshimika kwenye muziki wa Bongo Fleva. Kwenye kipindi chake kila msanii alitamani kufanya nae kazi, anasifika kwa majina mengi sana ila majina yake maarufu ni Mr Blue, Byser, Bablon na zamani alikuwa anajiita SIMBA na mengine kwa sasa akijiita NYANI ZEE. Jina lake halisi ni Herry Sameer Mzaliwa wa Dar Es Salaam. @mrbluebyser1988 ni miongoni mwa wasanii waliochonga njia kwenye soko la muziki wa Bongo Fleva. Kipi umekimisi kutoka na Blue Byser .

JAMVI LA HABARI
SPOTI
JUMATATU APRILI 22, 2024



**Mr Blue Byser ni msanii bora wa muda wote?**

# SIMBA, AZAM HAO KOMBE LA MUUNGANO

## >> Linafanyika baada ya miaka 20, Yanga yachomoa kushiriki



NA. MWANDISHI WETU

KWA mara ya kwanza baada ya miaka 20 Kombe la Muungano linarejea tena wakati ambao Taifa linasherehekea maadhimisho ya miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Taarifa ya Shirikisho la soka Tanzania (TFF) imesema TFF kwa kushirikiana na Shirikisho la Mpira wa Miguu Zanzibar (ZFF) zimetangaza kurejea kwa kombe hilo huku ikibainisha kuwa timu za Simba SC na Azam FC kutoka Tanzania Bara, zitashiriki katika Mashindano hayo ya mwaka huu yenye sura ya Uzinduzi wa Kombe hilo, huku kwa upande wa Visiwani timu shiriki ni mabingwa wa Zanzibar, KMKM pamoja na KVZ FC.

Mechi hizo zitachezwa Uwanja wa New Amaan Complex, Zanzibar kuanzia Aprili 23.

"TFF na ZFF tunawaomba Watanzania wote kushirikiana ili kufanikisha mashindano haya kwa ufanisi na ubora wa hali ya juu." imesema taarifa hiyo.

# Sergei Palkin: Chelsea hawajui kumtumia Mudryk

LONDON, UINGEREZA

MTENDAJI Mkuu wa Klabu ya Shakhtar Donetsk Sergei Palkin amemfunda Kocha Mkuu wa Chelsea Mauricio Pochettino, namna ya kumtumia Kiungo Mshambuliaji Mykhailo Petrovych Mudryk.

Mudryk alisajiliwa Chelsea Januari 15, 2023, kwa ada ya Pauni Milioni 62 sawa na Euro Milioni 70, na hadi sasa ameitumikia klabu hiyo ya jijini London katika Michezo 40 na kufunga mabao manne.

Palkin anaamini Pochettino hajafahamu namna ya



kumtumia Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 23, na ndio maana anashindwa kuonesha makeke yake kama alivyokuwa Shakhtar Donetsk.

"Mudryk ni mchezaji bora wa Ulaya, mchezaji wa kipekee. Ninaamini makocha wanahitaji kujifunza jinsi ya kumtumia na jinsi wachezaji wenzake wanahitaji kucheza naye.

"Ninapotazama akiwa anacheza pale Chelsea, karibu mashambulizi yote yanashuka upande wa kulia, sio kushoto, hakuzoea kucheza kwa namna hiyo, hivyo kuna haja kwa kocha wake kujifunza namna ya kumtumia."



**Ndumbaro: Tunajikita ujenzi wa viwanja AFCON 2027**

**IFAHAMIKE**

sasa serikali imejikita katika ujenzi na ukarabati wa viwanja vitakavyotumika katika Fainali za Mataifa ya Afrika 'AFCON 2027'.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA ADOR TANZANIA LTD, S. L. P 457822, DAR ES SALAAM